SportPesa
TZS. 433,401,140
CHEZA USHINDE JACKPOT
SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



## KESI YA SABAYA
Mahakama yakataa waraka wa utumishi

UKURASA 3


ama
ALHAMISI AGOSTI 19, 2021
AFYA NA MAZINGIRA

Ajenda kitaifa kuwalinda vijana na VVU hii hapa
Ukurasa 13

MAAJABU ZIWA MALIWE
Limejaa dagaa wenye mayai,viboko, mamba rafiki wa watu
Ukurasa 14

AUGUSTINE MASSAWE
**Bingwa watoto Muhimbili aliyeasisi mbinu ya 'kangaroo' iliyonusuru njiti**

Dokta Massawe atakumbukwa kwa kuokoa maisha ya maelfu ya watoto njiti. PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE.

Na Christina Mwakangale

TANZANIA inashika nafasi ya 20 duniani, kwa kuwa na watoto wanaozaliwa njiti wanaofikia 213,000 kila mwaka huku 40,000 wakipoteza maisha kutokana na matatizo mbalimbali ikiwamo shida ya upumuaji. Lakini pia ina asilimia 13 ya watoto wanaozaliwa kila mwaka wakiwa na uzito pungufu 'njiti,' hivyo kuongeza idadi ya vifo vya watoto wachanga hususan walio chini ya umri wa mwezi mmoja, ni kwa mujibu wa wataalam wa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH).

Mikakati ya kuokoa watoto njiti na kutumia mbinu ya kangaroo inayotumiwa na kitengo cha kulea watoto njiti cha Hospitali ya Taifa Muhimbili ikiwa ni kuiga namna ya malezi ya mnyama kangaroo, anayehifadhi mtoto wake katika mfuko wa asili uliopo nje ya tumbo na kumpa joto muda wote, haiwezi kuzisahau juhudi za daktari bingwa, Augustine Massawe.

Bingwa wa Watoto na Watoto Wachanga wa siku 0 hadi 28, katika Hospitali ya Muhimbili Dk. Massawe, amefariki mwisho mwa wiki iliyopita, lakini anakumbukwa kwa jitihada nyingi za kuokoa maisha ya njiti wa taifa hili.

"Kinamama wengi hususan ambao walipitia uzazi huu na kuwafanya kuhitaji huduma za kibingwa kutoka kwa wataalamu akiwamo Dk. Massawe, ili kuokoa maisha ya watoto wao, hawatamsahau," anasema Brigita Neema, wakati wa ibada ya kumuaga iliyofanyika Dar es Salaam, wiki hii.

Anasema hayo kwa sababu mtoto anayezaliwa chini ya miezi tisa na uzito mdogo itampasa kutumia kangaroo nyumbani au akiwa hospitalini na kuwekewa vifaa vya upumuaji, kazi aliyoifanya Dk. Massawe kuokoa maisha.

Makala hii ni kati ya nyingi ambazo Dk. Massawe alifanya mahojiano na gazeti hili, kuzungumzia mbinu mbalimbali za kuokoa njiti na kupunguza vifo akisema , wanaozaliwa na uzito mdogo ni rahisi kupoteza maisha ndani ya dakika 10, iwapo hawatakingwa na baridi na kupata nimonia ( homa ya mapafu)

Alisema watoto 260,000 huzaliwa nchini, wakiwa na uzito pungufu kutokana na sababu mbalimbali kipindi cha ujauzito, yakiwamo maradhi. Aliyasema haya kwenye maadhimisho ya siku ya watoto njiti duniani Novemba 17, 2020.

ALIZALIWA NJITI

Anasema aliwapenda watoto hao kwa sababu naye alizaliwa njiti... alikumbusha :"Asilimia 20 ya kinamama wanaozaa njiti wana umri mdogo. Nimefanya kazi hapa Muhimbili kwa miaka mingi nimehudumia binti wa miaka 15 ikijifungua njiti. Nimepewa jina la babu njiti, mimi nilizaliwa njiti mama yangu aliniambia hivyo."

Aliongeza kuwa utafiti uliofanywa mapema mwaka 2020 na Muhimbili ulionyesha kuwa mbinu ya kangaroo ilipunguza vifo vya watoto njiti kwa asilimia 25. Aidha kwa kushirikiana na Shirika la Afya Duniani (WHO), kwenye nchi tano za Tanzania, Ghana, Malawi, Nigeria na India, ilibainika kuwa mtindo huo utaokoa vifo

INAENDELEA UK.12

UKURASA 11

# Nipashe

Alhamisi Agosti 19, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0580677
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# Gwajima azidi kukaliwa kooni

**WAZIRI** asema lazima ashughulikiwe, amwandikia barua IGP Sirro ... *Endelea ukurasa 2*


IGP Simon Sirro


Dk. Dorothy Gwajima

## Wakuu SADC wakubaliana kuimarisha demokrasia

UKURASA 3

UKURASA WA 2

### LUGHA ILIVYOSAIDIA KUMALIZA MAUAJI IMANI ZA KISHIRIKINA

JESHI la Polisi Mkoa wa Njombe limesema limedhibiti mauaji yaliyohusishwa na imani za kishirikina baada ya kuanzisha mkakati wa elimu ikiwamo kumtumia askari...

UKURASA WA 4

### MWANAFUNZI ABUNI TEKNOLOJIA YA KUUA WADUDU MASHAMBANI

MWANAFUNZI wa kidato cha kwanza Shule ya Sekondari ya Ufundi ya Ifunda mkoani Iringa, Isaya William (14) amebuni roboti ambayo itatumika na wakulima...

## Maelfu wajitosa kupima DNA uhalali wa watoto

UKURASA 2

MICHEZO NDAYIRAGIJE, HERERIMANA WALA SHAVU LIGI KUU BARA UK. 23
MAONI, KATUNI UK.6

HABARI KITAIFA

## Lugha yamaliza mauaji Njombe

**Na Romana Mallya**

JESHI la Polisi Mkoa wa Njombe limesema limedhibiti mauaji yaliyohusishwa na imani za kishirikina baada ya kuanzisha mkakati wa elimu ikiwamo kumtumia askari polisi anayejua lugha za makabila yote yaliyomo mkoani humo kufikisha ujumbe.

Januari 2019, kulitokea mauaji ya watoto 10 mkoani humo huku miili ya watoto hao ilikutwa ikiwa imekatwa koromeo na sehemu za siri na kusababisha serikali kuunda timu ya uchunguzi.

Katika mahojiano maalum na Nipashe hivi karibuni kuhusu matukio hayo, Kamanda wa Polisi mkoani humo, Hamis Issa, alisema kuwa baada ya kushamiri kwa matukio hayo, Jeshi la Polisi kuanzia Januari mwaka huu liliandaa mikakati mipya ya kuyatokomeza.

"Kilichotokea ni kwamba kila tukio likitokea tulipomkamata mtuhumiwa na kumhoji anakiri kutenda kosa, Jeshi la Polisi tulibaini kuna tatizo la uelewa katika familia na imani za kishirikina zinawafanya wengine kukatishwa uhai," alisema.

Kamanda Issa alisema kuanzia Januari mwaka huu waliweka mkakati maalum wa kutembelea kata kwa kata kutoa elimu kwa wanakijiji inayolenga waachane na imani hizo walizonazo.

Kamanda Issa alisema wanapokwenda kutoa elimu huwa wanaambatana na watu wa dawati la jinsia, dawati linalohusiana na mauaji la mkoa, askari wa usalama barabarani, viongozi wa mila, ustawi wa jamii na viongozi wa maeneo husika.

Alisema kuwa katika utoaji elimu huwa wanazunguka na askari polisi ambaye ana uwezo wa kuongea lugha zote za makabila ya Mkoa wa Njombe ambaye husaidia pale wanaopobaini wanakijiji hawaelewi Kiswahili hasa vijijini.

"Mfano, vijijini tukiwa tunaongea Kiswahili na unaona wanakijiji hawaelewi, hakuna maswali, huyu askari polisi husaidia kuongea nao kwa lugha ya eneo husika, akiongea nao unaona wananchi wanamsikiliza kwa makini mpaka wanatikisa kichwa, hapo tunabaini elimu imewafikia," alisema.

Kamanda huyo alisema tangu wameanza kutoa elimu, kwa ujumla matukio yamepungua na wanaamini mkakati huo umesaidia na utakuwa endelevu.

# Gwajima azidi kukaliwa kooni

**Na Richard Makore**,

MWANZA

WAZIRI wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Doroth Gwajima, ameendelea 'kumkalia kooni' Askofu Joseph Gwajima kwa kumtaka athibitishe madai yake ya kiongozi wa serikali kuhongwa ili kuruhusu chanjo ya UVIKO-19 nchini.

Amesema amekamilisha taratibu zote za kisheria ikiwamo kuandika barua rasmi kwa vyombo vya usalama ili vianze kumhoji Askofu Gwajima.

Juzi Dk. Dorothy aliomba vyombo vya usalama kumhoji Askofu Gwajima, lakini Mkuu wa Jeshi la Polisi (IGP), Simon Sirro, alisema jeshi hilo haliwezi kufanya kazi hiyo bila kupata barua rasmi kutoka katika mamlaka husika.

Akizungumzia kauli hiyo ya IGP Sirro, Dk. Dorothy alisema kiongozi huyo wa Jeshi la Polisi yupo sahihi kwa kuwa vyombo vya usalama haviwezi kuanza kumhoji mtu bila kupata malalamiko rasmi kutoka kwa mlalamikaji ambaye ni yeye.

Akijibu maswali ya waandishi wa habari baada ya kuzungumza na watumishi wa Sekta ya Afya pamoja na viongozi mbalimbali wa serikali jijini Mwanza, waziri huyo alisema hakuagiza Askofu Gwajima akamatwe bali alitaka aitwe na kuhojiwa.

"Juzi nikiwa Butiama niliagiza vyombo vya usalama kumhoji Askofu Gwajima ili athibitishe madai yake kwamba viongozi wa serikali wamehongwa ili kuruhusu kuingiza chanjo ya UVIKO-19," alisema.

Alisema anataka Askofu Gwajima aitwe na kuhojiwa ili aeleze nani kahongwa, lini alihongwa, wapi alipewa fedha hizo na zilikuwa kiasi gani.

Kuhusu upotoshaji wa chanjo ya UVIKO-19, waziri huyo alisema kuna watu wengi wanapotosha suala hilo na kwamba kila mtu mwenye simu, atafute habari zake na kuzisoma ili afanye uamuzi badala ya kusikiliza mambo ya watu.

Dk. Dorothy alisema mtu akichanjwa ni rahisi mwili wake kupambana na ugonjwa wa corona kama ukimpata kuliko yule ambaye hajachanja.

"Wengi hawakusikiliza kipindi cha awamu ya tano, ndiyo maana wanauliza mbona mlisema hivi, Hayati Rais John Magufuli katika hotuba yake alisema msiwe mnakimbilia chanjo hadi mjiridhishe, hakusema msichanje," alisema.

Waziri huyo alisema kuna watu wanatembea na kivuli cha Hayati Rais Magufuli kwa kuwa na ajenda zao zinazopotosha.

Akizungumzia tiba asili, alisema chanjo haifuti tiba hizo na kuwapiga marufuku watu wanaogeuza Wizara ya Afya kuwa ajenda ya kisiasa.

Kuhusu takwimu za vifo vilivyotokana na ugonjwa wa corona, Dk. Dorothy alisema bado zinaandaliwa na muda siyo mrefu zitatolewa kwa nchi nzima.

"Hizi takwimu tunazo, zikiwa tayari zitatolewa kwa nchi nzima kwa sababu zipo wazi na kila mtu ataziona na kuzisoma," alisema.



Rais Samia Suluhu Hassan akiwa na Rais wa Zimbabwe, Emmerson Mnangagwa (katikati), pamoja na Mwenyekiti mpya wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), Rais wa Malawi Lazarus Chakwera (kushoto), wakati wa Mkutano wa 41 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa jumuiya hiyo, uliomalizika jijini Lilongwe, Malawi jana. **HABARI UK. 3. PICHA: IKULU**.

# Maelfu wajitosa kupima DNA uhalali wa watoto

**Na Mary Geofrey**

MAABARA ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA) imebainisha kuwa katika kipindi cha miaka minne kuanzia 2018 hadi mwaka huu, imefanikiwa kuchunguza sampuli za vinasaba vya binadamu 4,457 ili kubainisha uhalali wa watoto kwa wazazi.

Vilevile, imesema imechunguza sampuli 153 za majanga ya ajali ili kutambua miili ya waathirika ikiwamo ajali ya lori la mafuta iliyotokea eneo la Msamvu mkoani Morogoro Agosti 10, 2019 na kuua watu zaidi ya 100.

Mkemia Mkuu wa Serikali, Dk. Fidelice Mafumiko, alibainisha takwimu hizo jijini Dar es Salaam juzi katika hafla ya uzinduzi wa bodi ya pili ya mamlaka hiyo, uliofanywa na Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima.

Dk. Mafumiko alitaja sampuli zingine za majanga ya ajali kuwa ni za meli, ndege, magari, kuangukiwa na majengo; kulipukiwa na bomu pamoja na kuzama majini.

Dk. Mafumiko alisema pia wanafanya uchunguzi wa sampuli ili kuwezesha matibabu ya upandikizaji wa figo na utambuzi wa jinsi tawala.

Anasema katika kipindi cha miaka minne mamlaka kwa kushirikiana na hospitali zinazotoa matibabu hayo ikiwamo Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), walichunguza jumla ya sampuli 48 ili kuwezesha matibabu ya upandikizaji wa figo.

"Kadhalika, tulichunguza sampuli 22 ili kuwezesha matibabu ya utambuzi wa jinsi tawala kwa watu waliozaliwa na jinsi mbili (jinsi tata)," alisema Dk. Mafumiko.

Dk. Mafumiko alisema pia wanasimamia utekelezaji wa sheria tatu ambazo ni pamoja na Sheria ya Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali ya Mwaka 2016.

"Sheria hii pamoja na kuweka utu wa kisheria wa majukumu yote yanayofanywa na mamlaka, inaongeza majukumu mengine mawili ya usimamizi na udhibiti wa maabara za kemia, sayansi jinai na vinasaba vya binadamu nchini ukiondoa maabara za tiba," alisema Dk. Mafumiko.

Alisema mamlaka inatoa kibali kwa kila mzigo wa kemikali unaoingizwa nchini ili kuwatambua waingizaji wa kemikali, aina, kiasi na matumizi pamoja na kufanya ukaguzi kwenye viwanda, maghala na maeneo yote ambapo kemikali zinatumika kwa namna yoyote ile.

Alifafanua kuwa katika kipindi cha miaka minne, GCLA imesajili jumla ya wadau 3,024 wanaojihusisha na biashara ya kemikali, kutoa vibali vya kuingiza kemikali nchini 146,247 na kukagua maghala na sehemu zinazohifadhi kemikali 6,352.

Dk. Mafumiko alisema katika kipindi hicho mamlaka imechunguza kwa kuzingatia utaratibu wa kisheria jumla ya sampuli 8,619 za vinasaba vya binadamu. Alitaja aina za sampuli kuwa ni zinazohusiana na makosa ya jinai, masuala ya kijamii, majanga na matibabu.

Alisema jumla ya wadau 21 wanaojihusisha na uchunguzi wa vinasaba vya binadamu wamekaguliwa na maombi yao yamefanyiwa kazi kwa ajili ya kukamilisha taratibu za usajili

Waziri wa Afya, Dk. Dorothy, aliipongeza bodi inayomaliza muda wake kwa kusimamia vyema utekelezaji wa majukumu yake kwa kipindi cha miaka mitatu.

Alisema katika kipindi hicho, bodi ilisimamia utekelezaji wa majukumu ya kila siku ikiwamo uchunguzi wa sampuli na vielelezo mbalimbali, mapato na matumizi, usajili wa wadau wa kemikali, ukaguzi wa maghala ya kemikali, utoaji wa vibali vya kemikali na utoaji wa elimu kwa umma.

## HABARI KITAIFA

# SADC wakubaliana kuimarisha demokrasia

**Na Mwandishi Wetu**

MKUTANO wa 41 Nchi na Serikali za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), umemalizika huku raia wa Botswana, Elias Mpendi Magosi, akiteuliwa kuwa Katibu Mkuu Mtendaji mpya.

Rais Samia Suluhu Hassan alikuwa mmoja wa washiriki wa mkutano huo uliomalizika jana nchini Malawi kwa nchi wanachama kutia saini makubaliano ya mkutano huo.

Katika mkutano huo, wakuu wa nchi wanachana walikubaliana kuendelea kushirikiana na kusaidiana katika sekta ya uchumi na kijamii na hasa nchi ya Zimbabwe.

Wakuu hao pia walikubaliana kuendelea kuhimiza mshikamano, masuala ya amani na kukuza demokrasia katika jumuiya hiyo na kuendelea kuongeza idadi za nchi wananchama.

Vilevile, walikubaliana kuwapa ushirikiano Mwenyekiti mpya wa SADC, Rais wa Malawi, Lazarus Chakwera, aliyekabidhiwa nafasi hiyo kuiongoza kwa kipindi cha mwaka mmoja na Katibu Mkuu Mtendaji wa jumuiya hiyo.

Magosi anakuwa Katibu Mkuu Mtendaji wa Sita wa jumuiya hiyo tangu nafasi hiyo ianzishwe mwaka 1994 kuchukua nafasi iliyoachwa na mtangulizi wake, Mtanzania Stergomena Tax aliyeshika wadhifa huo tangu mwaka 2013.

Sambamba na hilo, mkutano unatarajiwa kufanyika tena Agosti mwakani katika Jamhuri ya Demokrasia ya Congo ambako Rais wa nchi hiyo, Felix Tshikesedi, atakabidhiwa uenyekiti wa SADC kutoka kwa mwenyekiti wa sasa.

Jumuiya ya SADC inaundwa na nchi 16 ambazo ni Angola, Botswana, Comoros, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), Eswatini, Lesotho, Madagascar, Malawi, Mauritius, Msumbiji, Namibia, Seychelles, Afrika Kusini, Tanzania, Zambia na Zimbabwe.

# KESI YA SABAYA: Mahakama yakataa waraka wa utumishi

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

KESI ya unyang'anyi wa kutumia silaha inayomkabili aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya, na wenzake, iliendelea jana huku mahakama ikikataa kupokea waraka wa utumishi kama kielelezo.

Akihojiwa na Wakili wa Serikali, Baraka Mgaya, katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Arusha mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi Odira Amwora, Sabaya alidai kuwa Februari 9, mwaka huu majira yaa saa 11 jioni alikuwa maeneo ya soko kuu jijini Arusha.

Sehemu ya mahojiano hayo na Wakili Mgaya ni kama ifuatavyo:

**Wakili:** Tajia mahakama majina yako matatu

**Shahidi:** Lengai Ole Sabaya

**Wakili:** Iambie mahakama kati ya majina hayo la baba lipi, la ukoo lipi na lako lipi.

**Shahidi:** Lengai jina langu, Sabaya la baba na Ole la ukoo.

**Wakili:** Nitakuwa sahihi nikisema Lengai Ole au Sabaya Ole?

**Shahidi:** Hautakuwa sahihi.

**Wakili:** Tarehe 9/2/2021 majira ya saa 11 jioni wewe na wenzako mlikuwa wapi?

**Shahidi:** Arusha Market Street

**Wakili:** Majira ya saa ngapi ulikuwa Market Street?

**Shahidi:** Majira ya saa 12 tulifika hapo Market Street

**Wakili:** Market Street kubwa, sema eneo gani.

**Shahidi:** Siwezi sema wala sina mamlaka ya kutoa siri hiyo niliyopewa na mamlaka maalum ya kufanya kazi.

**Wakili:** Wakati unatoa ushahidi wako hapa ulisema uliongoza siku hiyo timu uliyokuwa nayo kwa Mohamed Saad, ni sahihi?

**Shahidi:** Nilisema nilielekeza hao watu wanaomhitaji mtu huyo ambaye simfahamu na walikuwa na 'details' zake.

**Wakili:** Ni kweli ulieleza mahakama ulifika dukani kwa Mohamed Saad ukawachukua uliowakuta na kwenda nao polisi?

**Shahidi:** Nilieleza tulifika dukani na hao watu hatukuwakuta, walikuwapo wauza duka ambao walienda polisi.

**Wakili:** Ni sahihi hao watu walipofika dukani kwa Mohamed Saad wewe ulikuwa nao?

**Shahidi:** Sio sahihi

**Wakili:** Shahidi wa kwanza alijitambulisha kama Mohamed Saad hapa mahakamani, ni sahihi?

**Shahidi:** Alijitambulisha hivyo ila hakuja na ushahidi wowote na simfahamu japo alijitambulisha.

Sabaya aliendelea kudai mahakamani kuwa baada ya kukamilika kwa operesheni yake aliyofanya, ilirushwa na vyombo vya ITV na YouTube.

**Wakili:** Jaribio la kutishiwa kuuawa ni moja kati ya makosa ya polisi wanayotakiwa kufanyia kazi?

Shahidi: Sina jibu hilo, polisi wanapaswa kujilibu.

**Wakili:** Mkuu wa Wilaya ni Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama, hivyo kuwa mkimbizi kwa wiki mbili eneo lako la kazi, ebu iambie mahakama nani alitaka kukuua?

**Shahidi:** Wapo na siwezi kuwataja, vyombo vya dola vilifanya hiyo kazi.

**Wakili:** Wewe upo hapa mahakamani kutokana na Bakari Msangi kutoa taarifa polisi. Je, wewe uliyetishiwa kuuawa, ulitoa wapi na kina nani waliokutishia?

**Shahidi:** Nimeeleza (taarifa) zipo kwenye vyombo vya dola siwezi kutoa taarifa hapa, wanalifanyia kazi.

Baada ya mahojiano hayo kumalizika, Sabaya alihojiwa na Wakili Felix Kwetukia na ilikiwa kama ifuatavyo:

**Wakili:** Unakabiliwa na mashtaka matatu, eleza shtaka lipi unatuhumiwa kuiba pochi.

**Shahidi:** Sijaona shtaka lenye pochi

Wakili: Hivyo unatuhumiwa kuiba zaidi ya Sh. milioni 2.7 katika shitaka la kwanza na shtaka la pili Sh. 390,000 na la tatu Sh. 31,000 pamoja na simu ya mkononi Tekno na hakuna pochi?

**Shahidi:** Hakuna

Baada ya mahojiano hayo alihojiwa na Wakili wa Serikali Mkuu, Tumaini Kweka, na ilikuwa hivi:

**Wakili:** Ninafikiri Julai 16 mwaka 2021 ulisomewa maelezo ya mashtaka haya.

**Shahidi:** Ndio

**Wakili:** Sifa za taa Tube Light ni zipi?

**Shahidi:** Sijui

**Wakili:** Hivyo wewe unafikiria taratibu kama Tube Light?

Kabla Sabaya hajatoa majibu kwa swali hilo, Wakili wa Utetezi, Dancan Oola, aliingilia kati na kuiomba mahakama kumwelekeza wakili huyo kujikita kwenye maswali ya msingi na sio kutoa kashfa za wazi kwa shahidi.

Alidai kuwa wapo mahakamani kwa masuala ya haki na asiwapeleke kwenye kashfa.

Baada ya hoja hiyo kutolewa, Wakili Kweka aliendelea kufanya mahojiano na kumwonyesha shahidi huyo (Sabaya) waraka namba moja wa mwaka 1998 wa ofisi ya Rais Utumishi unaolekeza majukumu, mipaka ya kazi na uwajibikaji wa wakuu wa wilaya na kumtaka kuusoma, suala lililozua malumbano ya kisheria.

Wakili wa Utetezi, Oola, alisimama na kupinga waraka huo kusomwa na shahidi huyo kwa madai kuwa hauna sahihi ya nani ameutoa na haujakamilisha kurasa kutokana na kuonyesha ukurasa wa 50 hadi 53 pekee.

Alidai kuwa kimsingi hawawezi kujua kama kitabu au waraka rasmi hivyo aliomba uletwe wote la usikubaliwe mahakamani huko.

Hoja hiyo ilipingwa na Wakili Kweka kwa madai kuwa waraka huo namba moja umekamilika na zipo nyaraka nyingi zinazoonyesha hazijasainiwa na zinatumika ili mradi zinaonyesha zimetoka kwa nani kama huo aliouonyesha.

Baada ya malumbano hayo ya kisheria, Hakimu Mkazi Mwandamizi Amwora alikataa ombi la Wakili wa Serikali kutumia waraka huo kwa kuwa haujatiwa saini.

Kisha shahidi aliendelea na mahojiano na Wakili Kweka.

Kesi hiyo ya jinai namba 105 ya mwaka inayomkabili Sabaya na wenzake wawili inaendelea kunguruma Mahakama ya Hakimu Mkazi Arusha na watuhumiwa wako katika Gereza Kuu Arusha kutokana na kesi hiyo kutokuwa na dhamana.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA NISHATI

MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)

## TAARIFA KWA UMMA

**(Imetolewa chini ya kifungu Na.19 cha Sheria ya Mamlaka ya Udhibitiwa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), Suraya 414 ya Sheria za Tanzania na Kanuni Na. 21(4) ya Kanuni za Mafuta (Biashara ya Jumla, Uhifadhi, Reja Reja na Matumizi Binafsi),Gazeti la Serikali Toleo Na. 817 la 2020)**

**TAARIFA** inatolewa kwa umma kwamba Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imepokea ombi la kubadili umiliki wa leseni na jina la kituo kama ifuatavyo: -

| | |
|---|---|
| **Jina la awali la kituo:** | Njake Enterprises & Oil Transport Ltd - Mianzini Petrol Station |
| **Nambari Ya Leseni:** | PRL-2018-069. |
| **Mahali Kituo Kilipo:** | Kiwanja Na. 88, Kitalu 'DD' Eneo la Mianzini, Wilaya ya Arusha Mkoani Arusha. |
| **Jina Linalopendekezwa:** | Milton Blasto Makundi – Mianzini Petrol Station |
| **Mmiliki Wa Awali:** | Njake Enterprises & Oil Transport Ltd |
| **Mmiliki Mpya:** | Milton Blasto Makundi |

Mtu yeyote mwenye maoni au pingamizi dhidi ya mabadiliko ya umiliki na majina ya leseni tajwa hapo juu, afanye hivyo kwa maandishi na kuwasilisha EWURA kwa anwani iliyotajwa hapa chini ndani ya siku kumi na nne toka tarehe ya tangazo hili.

**Mkurugenzi Mkuu,**
**Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji – EWURA**

216414502

## Waziri aponda mradi chumvi

**Na Thobias Mwanakatwe**

WAZIRI wa Madini, Dotto Biteko, ameuponda mradi wa kuzalisha chumvi katika Kijiji cha Itumbula, Momba mkoani Songwe wenye thamani ya Sh. bilioni 41, kwamba andiko lake limejaa uongo.

Alisema hayo juzi baada ya kutembelea mradi huo akiwa ameambatana na Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Omary Mgumba, Mbunge wa Momba, Conderster Sichalwe na kupewa taarifa na waatalam wa halmashauri ya wilaya.

"Katika jambo ambalo mimi sipendi ni kufanya siasa kwenye maisha ya watu. Ni bora uwaambie watu ukweli kuliko kuwapa ahadi hewa, ukilisoma andiko la mradi huu limejaa uwongo mwingi," alisema.

Biteko alisema kimsingi hakuna mtu au serikali inayoweza kuleta Sh. bilioni 41 kwa sababu imezungumzwa kuwa fedha hizo zitapatikana ndani ya miaka miwili kitu ambacho ni uongo na hakiwezekani.

"Uzalishaji waliouweka hapa wanasema watazalisha tani 1,126,000 watauza chumvi ikiwa haijawekwa kwenye mfuko tani 91,220 na ikiwa kwenye mifuko itauzwa tani laki moja, ukichukua hizo tani ukazidisha hupati Sh. bilioni 20 mwaka wa kwanza," alisema.

Biteko pia alihoji mradi huo ulikuwa unaendeshwa na wananchi kulikuwa na ulazima gani serikali kuwanyang'anya badala kuacha wananchi waunde vikundi halafu wapate mkopo wa kuuendesha.

Aliongeza kuwa Sh. milioni 500 ni fedha nyingi kwa mradi wa chumvi, hivyo kinachohitajika ni teknolojia ya jinsi ya kuchanjua chumvi msimu wote bila kujali mvua na zitawekwa mashine za kukausha.

Biteko alisema mambo ya mtu mmoja anajifungia Dar es Salaam anaandika mradi aaah aaah jamani tuoneane huruma, ni serikali gani yenye hela nyingi za kuchezea kiasi hicho wakati hakuna hata leseni.

"Ofisa Mipango hapa ananipiga fiksi. Andiko la mradi nalo limenipiga fiksi, unapigwa fiksi kuanzia asubuhi hadi jioni," alisema.

Naye Mkuu wa Mkoa Songwe, Mgumba, alisema wataalam wamejifedhehesha kwa mradi huo na kuagiza wasiwe wanapeleka maandiko yoyote juu kabla ya kuyapitisha wilayani na mkoani.

# Mwanafunzi abuni teknolojia ya kuua wadudu mashambani

**Na Mwandishi Wetu,** IRINGA

MWANAFUNZI wa kidato cha kwanza Shule ya Sekondari ya Ufundi ya Ifunda mkoani Iringa, Isaya William (14) amebuni roboti ambayo itatumika na wakulima kunyunyuzia dawa shambani, ili kujiepusha kupata magonjwa mbalimbali ikiwamo pumu.

Akizungumza jana na waandishi wa habari waliopo kwenye ziara ya kuangalia namna Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia inavyoendelea kuwasaidia wabunifu mbalimbali, mwanafunzi huyo alisema roboti hiyo itasaidia kusambaza dawa shambani, ili kuepuka mkulima kupata magonjwa.

"Nashiriki kutengeneza project (mradi) kwa kushirikiana na wenzangu ambao utasaidia kupuliza dawa mashambani, nitatumia roboti ambayo itasaidia kusambaza dawa katika mashamba, ili kuepukana na kupata matatizo mbalimbali wakati wa kupulizia dawa,"alisema.

Alisema roboti hilo litatumia ramani ya shamba kwa kutumia programu maalum ambayo itakuwa katika simu ya mkulima.

"Application hiyo itakuwa katika simu ya mkulima ambayo atatumia ramani ya shamba na roboti atakuwa anazunguka katika shamba, itasaidia kuokoa muda ataenda shambani na kumuepusha na maradhi mbalimbali na magonjwa kama pumu."

"Roboti atakuwa kama kigari fulani na kutakuwa na tenki juu na kutakuwa na bomba na kwenye matairi kutakuwa na minyororo kama ya pikipiki, kwa ajili ya kupita chini,"alisema.

Alisema itachukua wiki moja kukamilisha ubunifu huo, ambapo alisema malengo ni kusaidia sekta ya kilimo na kuhakikisha wakulima wanafanya kilimo cha kisasa.

Katika hatua nyingine, mwanafunzi wa kidato cha sita, Oscar Mletwa, amebuni kifaa ambacho kitakuwa kikitoa taarifa kwa utawala wa shule na matroni baada ya kutokea kwa janga la moto.

Alisema kwa miaka mitatu 2019, 2020 na 2021 shule nyingi zimeungua moto, ambapo chanzo chake ni wanafunzi kujitengenezea shoti juu ya madari.

"Nimetumia miezi sita kutengeneza, lengo langu nataka kuwa injinia mkubwa nchini, ili kuisaidia nchi katika mambo mbalimbali," alisema.

Mwalimu Mkuu wa Shule hiyo,Yusuphu Mwagala, alisema wanaendelea kuwaendeleza wabunifu hao kwa kuwaunga na taasisi mbalimbali za ubunifu pamoja na chama cha ubunifu na Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST).




Ofisa Rasilimali Watu wa Kampuni ya Vodacom Tanzania Plc, Gervas Mfubusa (kushoto), akizungumza na washiriki wa mafunzo ya TEHAMA, yaliyopewa jina la 'Code like a girl', mpango unaoendeshwa kupitia taasisi isiyo ya kiserikali ya dLab, jijini Dar es Salaam jana, ili kuhamasisha wasichana kupenda masomo ya sayansi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wafugaji wadai kutozwa faini bila risiti

**Na Pendo Thomas,** KIGOMA

WAFUGAJI jamii ya Wasukuma kutoka Kijiji cha Mgambazi wilayani Uvinza wamelalamikia kuvamiwa na Askari wa Wanyamapori waliokusanya ng'ombe majumbani na kuwalazimisha kulipa zaidi ya Sh. milioni 30 pasipo kupewa risiti.

Wafugaji hao wanadai kuwa walivamiwa na askari hao na kuchukuliwa mifugo yao kwa madai ya kuchanganyika na wakulima na wafugaji.

Kwa mujibu wa wafugaji hao, kutokana na uporwaji wa mifugo yao na vitendo vya vitisho walivyofanyiwa, wameiomba serikali kuingilia kati, ili warudishiwe fedha zao.

Hollo Machia, mmoja wa wafugaji hao, alisema siku ya tukio, askari walifika nyumbani kwake wakiwa na silaha wakamwambia aswage ng'ombe kupeleka eneo la jirani ambalo kulikuwa na mifugo ya watu wengine.

Alisema baada ya agizo hilo, alilazimika kutekeleza kwa kuogopa kujeruhiwa na silaha walizokuwa wamebeba.

Mfugaji mwingine, Kazinza Malekana, alisema siku ya tukio alijaribu kuuliza uhalali wa wanachokitekeleza, lakini aliwekwa chini ya ulinzi na kuambiwa hapaswi kuuliza sana maswali ikiwamo kutishiwa silaha.

"Tulijitetea sana lakini wakatuambia msipotoa hizo pesa mifugo yote tunaondoka nayo kuelekea ofisi za wilaya, hivyo hatukuwa na namna ikabidi tutekeleze maagizo yao," alisema.

Saamoja Madoshi, Mwenyekiti wa Wafugaji katika Kitongoji B Mgambazi, alisema mbali na Sh. milioni 30 kutozwa kama faini, kuna takribani ng'ombe 70 walipotea, hivyo wanaomba serikali isaidie kurudishwa mikononi mwao.

"Tunashangaa kwa nini tumetozwa faini kwa makosa tusiyoyajua na bila kupewa risiti, alisema.

Baada ya tukio hilo, alisema waliamua kufuatilia katika ofisi ya wilaya kufahamu undani wa tukio hilo kwa kuwa wahusika waliwaambia wanatekeleza agizo kutoka wilayani.

Mkuu wa Wilaya ya Uvinza, Hanafi Msabaha, alisema alipata malalamiko hayo kutoka kwa wafugaji na tayari amechukua hatua za haraka za kuchunguza madai hayo.

Alisema opereshani halali aliyokuwa na taarifa yake ni ukaguzi wa maeneo ya hifadhi tofauti na malalamiko yaliyo mfikia.

Msabaha alibainisha kuwa wameanza kuchunguza uhalali wa mifugo ilipo kwa kuwa wafugaji wanasema ilikuwa kwenye makazi yao na walioendesha doria wakisema ilikuwa hifadhini. Pia alisema wanachunguza suala la uhalali wa faini walizotozwa na kama kweli fedha hizo zimeingia serikalini.

"Kutokana na malalamiko hayo nimesimamisha opareshani hiyo hadi tutakapojiridhisha kama ilifuata utaratibu au la," alisema.

HABARI KITAIFA

# Ndugai ataka elimu wanaoogopa sensa

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

SPIKA wa Bunge, Job Ndugai, ameitaka Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali kutoa elimu kwa wananchi juu ya umuhimu wa Sensa ya Watu na Makazi ili kuondokana na imani potofu kwa baadhi ya makabila yanayokataa kuhesabiwa kwa kuogopa kufa.

Ndugai aliyasema jana jijini hapa kwenye kikao cha uhamasishaji wa utoaji elimu ya sensa hiyo inayotarajiwa kufanyika Agosti, mwakani nchini.

Alisema elimu isipotolewa ipasavyo, itasababisha kukwamisha sensa hiyo kwa kuwa kuna baadhi ya makabila mila zake zinakataa kuhesabu watu wake au mifugo yao.

"Kwa jambo la kujitokeza kwa watu kuhesabiwa ni jambo muhimu sana, kuhesabiwa si jambo rahisi kwa sababu zipo baadhi ya nchi hazina sensa kwa sababu haziamini katika kuhesabiwa lakini sisi tunashukuru tumeendelea na zoezi hilo kwa miaka mingi.

"Kwa mfano, sisi wagogo hapa ukitaka kuhesabu mifugo ya mtu yaani akuambie ana mifugo mingapi na ngombe na mbuzi wangapi, utapata tabu sana, hata ukimuuliza mtu una watoto wangapi au wake wangapi, hatakupa takwimu sahihi kwa sababu ni utamaduni wetu, tuko hivyo, hivyo zoezi hili linataka elimu itolewe," alisema.

Alisema kuwa elimu ikitolewa itaondoa mawazo na imani potofu iliyopo kwa baadhi ya makabila nchini yanayokataa kuhesabiwa kwa madai ya kuogopa kufa.

Spika mstaafu Anne Makinda ambaye pia ni Kamishna wa Sensa nchini, alisema kuna umuhimu Tanzania kupata idadi ya watu wake katika kupanga maendeleo ya watu wake na kukuza uchumi.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka, alisema kikao hicho kilishirikisha viongozi wa dini, siasa, walemavu, wafanyabiashara na madereva bodaboda.

Alilitaja kundi lingine kuwa ni la viongozi wakuu wa mkoa ambao ni wabunge, wakuu wa wilaya, wenyeviti wa halmashauri, wakurugenzi na maofisa mipango ili kuhakikisha wanapata elimu hiyo na jumla ya washiriki 500 wamehudhuria kikao hicho.

Awali, Mtakwimu Mkuu nchini, Dk. Albina Chuwa, alisema serikali inakusudia kufanya sensa ya aina yake ya watu na makazi ya mwaka 2022 kutokana na kukusanya madodoso mengi muhimu ambayo yatasaidia nchi katika maendeleo ya watu wake.

Alibainisha kuwa sensa hiyo itatumia vishikwambi katika kukusanya taarifa mbalimbali kwa ajili kukukidhi mahitaji mengi ya serikali ili kuwahudumia wananchi.

Alisema sensa hiyo itahitaji taarifa za idadi ya watu walioajiriwa na kujiajiri kujua idadi ya watu wasio na ajira nchini.

# RC ahamasisha upimaji wa VVU kwa wanaume

**Na Mwandishi Wetu,** LINDI

MKUU wa Mkoa wa Lindi, Zainab Telack, amesema miongoni mwa sababu zinazochangia ongezeko la maambukizi ya Virusi vya UKIMWI mkoani humo ni shughuli za kiuchumi, mila na desturi.

Kufuatia hali hiyo, kiongozi huyo ameitaka Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS) kuendeleza kampeni ya wanaume kupima afya zao kwa kuwa suala la upimaji bado ni tatizo.

Telack aliyasema hayo jana alipozungumza na Mkurugenzi Mtendaji wa TACAIDS, Dk. Leonard Maboko, aliyezuru kwa ajili ya ufatiliaji na tathimini ya afua za VVU na UKIMWI zinazotekelezwa katika mkoa huo.

Alisema pamoja na uwapo wa maeneo hatarishi yanayosababishwa na shughuli za kiuchumi, mila na desturi zinazofanyika katika mkoa huo, wanaume hawajitokezi kupima afya zao na kusababisha maambukizi kwa wenza wao kwa kuwa hawajui hali zao za maambukizi ya VVU.

"Uwezekano wa maambukizi kuongezeka Lindi ni mkubwa kutokana na uwapo wa wageni hasa katika maeneo ya vijijini ambapo, pia elimu ya VVU na UKIMWI haijafika na ngono zinafanyika kwa wingi," alisema.

Alishauri wadau wanaotekeleza afua za VVU na UKIMWI katika Mkoa wa Lindi wasimamiwe na kuratibiwa vizuri, ili wafike hadi kwenye maeneo hatarishi ambayo yanaweza kuleta ongezeko la maambukizi mapya ya VVU.

"Tukiacha hali hii iendelee katika mkoa wetu, tatizo litakuwa kubwa kwa kuwa wanaume wanaofanya ngono na wanawake hao bado watakuwa na wanawake wengine, kwa kufanya hivyo, maambukizi yatazidi kuwa makubwa," Aidha,

Dk. Maboko aliagiza waratibu wa UKIMWI wa mkoa huo kuhakikisha wanafanyia kazi kero zilizoainishwa, ili kuhakikisha wanapunguza maambukizi mapya na ifikapo mwaka 2030 wawe wamefikia lengo la kidunia la kuwa na maambukizi mapya sifuri, unyanyapaa sifuri na vifo vitokanavyo na UKIMWI sifuri.

Katika ziara yake, Mkurugenzi wa TACAIDS alikutana na Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Ruangwa, Rashid Namkulala, na watendaji wengine ambapo alitaka kujua hali ya upatikanaji na usambazwaji wa kondomu katika halmashauri hiyo.

Dk. Maboko alielezwa kuwa tayari makasha 308 yamepokewa na kusambazwa katika maeneo ya vipaumbele ambapo tayari kote kuna kondomu na wananchi wanaendelea kupata huduma hiyo ya kinga ya maambukizi mapya ya VVU.

Mratibu wa UKIMWI wa Halmashauri ya Ruangwa, Mariam Kimaro, alisema Rauangwa inakabiliwa na mwingiliano wa watu kutokana na machimbo ya madini, minada, kilimo cha ufuta na miradi ya maendeleo inayoendelea katika halmashauri hiyo.

Alisema kutokana na maeneo hatarishi hayo, elimu inaendelea kutolewa kwa wananchi licha ya kuwapo kwa tatizo la rasilimali fedha.

EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

**MAOMBI YA TAARIFA YA KUONYESHA NIA YA KUTOA HUDUMA YA KUANDAA MPANGO KAZI WA ZIADA WA UHAMISHAJI WA WATU NA MAKAZI PAMOJA NA MPANGO WA UREJESHAJI WA UWEZO WA KUJIKIMU KWA AJILI YA MRADI WA BOMBA LA MAFUTA GHAFI LA AFRIKA MASHARIKI (EACOP)**
**KUMBUKUMBU NA: 0010006870**

TOTAL East Africa Midstream B.V (Kampuni) Tanzania, kampuni ya kimataifa ya nishati, inaalika makampuni/taasisi yenye utaalamu na uzoefu katika Uhamishaji wa Watu na Makazi Pamoja na Urejeshaji wa Uwezo wa Kujikimu kutuma nia ya kutoa huduma katika Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP).

Mradi wa EACOP unajumuisha ujenzi na uendeshaji wa bomba litakalofukiwa chini linalokatisha mipaka ya nchi mbili na litakalo safirisha Mafuta kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda mpaka pwani ya Mashariki ya Tanzania kwa ajili ya kusafirisha Mafuta hayo katika masoko ya kimataifa. Bomba litaanzia Kabaale katika Wilaya ya Hoima, nchini Uganda, mpaka Chongoleani, Mkoa wa Tanga nchini Tanzania. Urefu wa bomba ni karibia kilomita 1,443, kati hizo kilomita 1,147 zitakuwa nchini Tanzania. Ardhi imeshatwaliwa katika rasi ya Chongoleani kwa ajili ya ujezi wa kitua cha kuhifadhia mafuta kilicho pembezoni mwa bahari na kugusa jamii ambazo zinategemea ardhi pamoja na bahari ili kuweza kujikimu.

**MAELEZO MAFUPI YA MAWANDA YA HUDUMA:**

Kampuni inahitaji huduma kutoka kwa makampuni/taasisi yaliyobobea/iliyobobea katika Uhamishaji wa Watu na Makazi Pamoja na Urejeshaji wa uwezo wa kujikimu kwa lengo la:

- Kuandaa Mpango Kazi wa Uhamishaji wa Watu na Makazi (RAP) wa ziada kwa ajili ya Waguswa wa Mradi waliopo katika jamii inayoishi kwenye Rasi ya Chongoleani.
- Kufanya tathmini ya uwezo wa kujikimu (katika matumizi ya ardhi Pamoja na bahari) katika jamii.
- Kuandaa Mpango wa Urejeshaji wa Uwezo wa Kujikimu (LRP) kwa ajili ya Jamii ya Rasi ya Chongoleani iliyoguswa na Mradi.

**VIGEZO MUHIMU:**

Makampuni yanayoonyesha nia yanaalikwa kutuma maombi pamoja na nyaraka zifuatazo:

- Uthibitisho wa kuandaa Mipango Kazi ya Uhamishaji wa Watu na Makazi Pamoja na Mipango ya Urejeshaji wa Uwezo wa Kujikimu katika miradi ya viwanda barani Afrika.
- Uthibitisho wa uzoefu wa kusanifu mipango ya uhamishaji wa watu na makazi pamoja na mipango ya urejeshaji uwezo wa kujikimu katika miradi mikubwa ya ujenzi inayodhaminiwa.
- Afisa anayependekezwa pamoja na wataalam wa maswala ya ardhi na uwezo wa kujikimu katika matumizi ya ardhi na bahari pamoja na uzoefu wao katika kutoa huduma kwenye eneo husika.
- Uthibitisho wa usajili wa watekelezaji wa ngazi za juu katika taasisi za kitaaluma za Kitanzania au shirikisho.
- Usajili katika Kanzi Data ya Watoa Huduma wa Ndani ya EWURA (LSSP) katika kipindi cha kuwasilisha majibu ya nia kwa ombi hili yanahimizwa.

Makampuni zenye nia, uwezo na rasilimali za kutoa huduma zilizotajwa hapo juu zinatakiwa kutuma taarifa ya kuonyesha nia iliyoandaliwa kwa lugha ya kiingereza pamoja na nyaraka tajwa kupitia barua pepe: **robin.schroh@external.totalenergies.com** (ukubwa usiozidi MB20) hadi kufikia saa **11:00 jioni** Majira ya Afrika Mashariki, tarehe **25 Agosti 2021.**

**Muhimu: Kwa ajili ya kutengeneza orodha ya makampuni ya Awali yenye vigezo, Mradi wa EACOP utapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na makampuni yenye nia. Mwaliko kwa Makampuni kutuma maombi ya zabuni utatumwa kwa Makampuni ya Awali yenye vigezo baada ya makampuni hayo kusaini Makubaliano ya Utunzaji wa Taarifa (NDA).**

216414602

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Elimu kuhusu sensa kwa umma muhimu

**SENSA** ya watu na makazi ni suala muhimu sana kwa kila taifa. Kutokana na umuhimu huo, ndio maana ni takwa la kisera na kisheria.

Umuhimu wa sensa unatokana na kutoa takwimu halisi za idadi ya watu katika nchi, hivyo kuisaidia serikali katika kupanga mipango yake ya maendeleo, ukihusisha huduma za jamii.

Kwa maneno mengine, wataalamu wa mipango wanapokuwa na takwimu sahihi za idadi ya watu, unakuwa rahisi kwao kupanga mipango ambayo inawalenga watu wote, zikiwamo huduma.

Kwa mfano, serikali haiwezi kuandaa bajeti kwa kutenga fedha za ujenzi wa miundombinu ya elimu, afya, maji, barabara, madaraja na huduma nyingine muhimu bila kuwa na takwimu halisi zinazohusu idadi ya watu pamoja na makazi.

Hata hivyo, katika nchi yetu baadhi ya wananchi wamekuwa na mtazamo hasi kuhusu sensa na matokeo yake kuwa wagumu kujitokeza kuhesabiwa, hivyo kukwaza malengo ya sensa.

Kuna wakati baadhi ya jamii zimekuwa zikitoa masharti kwa serikali iyatekeleze ili zikubali kuhesabiwa, ikiwamo kudai kupewa vyakula bila kujua kuwa kufanya hivyo ni kukwaza zoezi hilo lenye lengo zuri la kuwapatia huduma stahiki katika maendeleo kwa ujumla.

Lakini kwa mtazamo wetu tunaona kuwa hali hiyo inasababishwa na kukosekana kwa elimu ya kutosha juu ya umuhimu wa sensa kwa maendeleo ya wananchi na taifa kwa ujumla.

Kwa kuona tatizo hili pengine ndio maana Spika wa Bunge, Job Ndugai, ameitaka Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali kutoa elimu kwa wananchi juu ya umuhimu wa Sensa ya Watu na Makazi ili kuondokana na imani potofu kwa baadhi ya makabila yanayokataa kuhesabiwa, ikiwamo kuogopa kufa.

Ndugai aliyasema hayo jana jijini hapa kwenye kikao cha uhamasishaji wa utoaji elimu ya sensa hiyo inayotarajiwa kufanyika nchini Agosti, mwakani.

Alisema elimu isipotolewa ipasavyo, itasababisha kukwamisha sensa hiyo kwa kuwa kuna baadhi ya makabila mila zake zinakataa kuhesabu watu wake au mifugo yao.

Alisema kuhesabiwa ni jambo muhimu sana, na kwamba kuhesabiwa si jambo rahisi kwa sababu zipo baadhi ya nchi hazina sensa kwa sababu haziamini katika kuhesabiwa, ingawa jambo la kushukuru ni kuwa Watanzania tumeendelea na zoezi hilo kwa miaka mingi.

Alisema elimu ikitolewa itaondoa mawazo na imani potofu iliyopo kwa baadhi ya makabila nchini yanayokataa kuhesabiwa.


Spika mstaafu, Anne Makinda, ambaye ni Kamishna wa Sensa nchini, alisema kuna umuhimu Tanzania kupata idadi ya watu wake katika kupanga maendeleo ya watu wake na kukuza uchumi.

Kwa kuwa nchi yetu imebaki na takribani mwaka mmoja kabla ya sensa hiyo kufanyika, sisi tunazishauri mamlaka husika za serikali kutoa kipaumbele kwa elimu ya umma, kwa lengo la kuwawezesha wananchi wengi kujua manufaa ya kuhesabiwa.

Ofisi Kuu ya Takwimu (NBS) hainabudi kuweka mipango na mikakati ya kutoa elimu hiyo sambamba na kufanya uhamasishaji kupitia viongozi wa dini, siasa, mashirika yasiyo ya kiserikali na vyombo vya habari. Tunaamini kuwa hilo likifanyika mapema, bila shaka wananchi wengi watakuwa na uelewa na mwitikio wa kuhesabiwa utakuwa mkubwa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Mtandao umekuja wakati mwafaka kukomesha biashara ya binadamu



Na Sabato Kasika

**USAFIRISHAJI** haramu wa binadamu unaowaathiri zaidi wanawake, wasichana na watoto unawasukuma wadau kuanzisha mtandao wa kupambana na biashara hiyo inayoelekea kushamiri Tanzania.

Baadhi ya walioguswa na kuunda mtandao huo ni asasi mbalimbali zikiwamo za kidini, vyuo vikuu vyama vya kutetea abiria na vya wamiliki wa vyombo vya usafiri ambao wameungana na kupanga kutoa elimu ya kusaidia jamii kuachana na kusafirisha na kuuza binadamu wenzao.

Mtandao wa Tanzania Network Against Human Trafficking (TANAHUT), kwa mujibu wa Mwenyekiti Edwin Mugambila, unapambana kutokana na biashara hiyo kuumiza maelfu ya watu na kuwaachia athari kubwa kwenye maisha.

Anasema wahusika hasa wasichana huchukuliwa vijijini kwa ahadi za kupelekwa mijini kufanya kazi, lakini wakifikishwa badala ya kufanya kazi walizoahidiwa, zikiwamo za ndani hutumikishwa kingono kwenye madanguro, hali ambayo inawaweka kwenye hatari ya kukumbwa na magonjwa ya ngono, kutumia dawa za kulevya na vileo na kushiriki uhalifu.

Kutokana na mazingira hayo, mtandao huo unajipanga kuanza kutoa elimu mwishoni mwa mwezi huu, katika maeneo yote ya Dar es Salaam ambayo biashara hiyo ya ngono hufanyika.

Mbali na Dar es Salaam wadau wa mtandao huo wengine watakuwa jijini Dar es Salaam na kisha wataingia maeneo ya vijijini ambako wasichana na wanawake huchukuliwa na kupelekwa mijini kwa ahadi ya kupewa kazi.

Kwa mujibu wa Mugambila, elimu hiyo itatolewa kwa muda wa miaka mitano, na baada ya hapo, watafanya tathmini ya elimu hiyo, kisha matokeo ndiyo yatawapa picha halisi ya mafanikio, changamoto na walipokwama.

Muungwana naunga mkono mipango na mkakati ya mtandao huo, ili kunusuru kundi hilo dhidi ya hatari za magonjwa, dawa za kulevya, athari kisaikolojia na kuwaharibia maisha na kuvunja utu wao.

Jijini Dar es Salaam yapo baadhi ya maeneo ambayo biashara hiyo imekuwa ikifanyika, inawezekana baadhi ya wahusika ni wale waliotolewa vijijini kwa ahadi ya kuja jijini kufanya kazi na kujikuta wakiishia kutumikishwa kwenye biashara ya ngono na uhalifu.

Hivyo, kuwapo kwa elimu hiyo kunaweza kuwajengea uelewa wahusika na hatimaye wakaacha kuwa katika mazingira hayo hatarishi ambayo huenda baadhi yao wanadhani ni ya kawaida na kumbe ni hatari.

Kimsingi, biashara hiyo haramu ya kusafirisha binadamu hairuhusiwi, ndiyo maana wiki iliyopita, Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu Dar es Salaam, iliwahukumu watu watatu kwenda jela miaka 25 baada kukutwa na hatia ya kujihusisha na jinai hiyo.

Wakati mtandao huo ukijiandaa kufanya kazi baadhi ya wahusika wakinaswa, ninadhani ipo haja ya wananchi kila mmoja kwa nafasi yake kuunga mkono na kushiriki kunusuru wengine wasiingizwa kwenye kadhia hiyo inayohatarisha maisha.

Si vibaya kutoa taarifa kwa polisi, uhamiaji na ustawi wa jamii, vijiji na viongozi wa mitaa iwapo mtu kwenye eneo analoishi au kufanyia kazi ataona kuna dalili za kuwapo kwa biashara hiyo ili kusaidia kundi hilo kuwa salama.

Hata huko vijijini ambako inaelezwa kuwa wasafirishaji wapo na hutoa ahadi tele za kazi na kumbe ni kutumikisha mabinti kwenye biashara ya ngono, ni vyema elimu ikatolewa zaidi kwa wazazi na walezi nao pia wakawa sehemu ya kutoa taarifa.

Inawezekana huwa wanaruhusu watoto wao kuchukuliwa kwenda mijini wakiamini kwamba, wakifika na kuanza kazi watapata mishahara ya kuwawezesha kwa chochote.

Ninadhani kwamba, watoto, wazazi na walezi hao wakielemishwa, watakuwa makini na watu hao wanaowafuata kwa ahadi ya kazi na kumbe lengo ni kuwatumikisha kwenye biashara ya ngono.

Hivyo, si vibaya kila mmoja kuhakikisha uhalifu huo unakomeshwa, lakini wahusika kujengewa uwezo wa kujitambua ili wawe makini na wale wote wanaojihusisha na biashara hiyo ambayo inaharibu utu wa mtu.

## TANGAZO

MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA
ISO 9001: 2015 IMETHIBITISHWA

TANESCO
We light up your life

# TAARIFA KWA UMMA

## UTEKELEZAJI WA UKUSANYAJI KODI YA MAJENGO KWA KUTUMIA NJIA YA UNUNUZI WA UMEME

Serikali imeanza utekelezaji wa kukusanya kodi ya majengo kwa kutumia mfumo mpya wa ukusanyaji kupitia ununuzi wa umeme. Utekelezaji huu utaanza rasmi tarehe **20 Agosti, 2021** na unafanyika chini ya usimamizi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kwa kushirikiana na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) ukihusisha mita za aina zote za umeme.

Utaratibu huu unafanyika kufuatia marekebisho ya Sheria ya Kodi ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa, Sura ya 289 iliyopitishwa na Bunge la Bajeti la mwaka 2021 ambapo viwango vya kodi ya majengo vimebadilishwa.

Viwango hivyo kwa sasa ni **shilingi 12,000** kwa kila jengo la kawaida ndani ya kiwanja kutoka **shilingi 10,000** iliyokuwa ikitozwa awali, na **shilingi 60,000** kwa kila sakafu ya ghorofa kutoka **shilingi 50,000.** Hata hivyo, kwa upande wa Halmashauri za Wilaya na Miji Midogo, nyumba za ghorofa bila kujali idadi ya sakafu zitatozwa **shilingi 60,000.**

Kwa njia hii mpya ya ukusanyaji wa kodí, kíla mnunuzi wa umeme atakatwa **shilingi 1,000** kwa mwezi kwa nyumba ya kawaida na **shilingi 5,000** kwa mwezi kwa kila sakafu ya ghorofa. Kwa wale wanaotumia mita za Ankara watalipa kodi hii kwa pamoja katika Ankara ya mwezi.

Kwa wamiliki ambao majengo yao hayajapata umeme, wataendelea kulipa kodi hiyo kwa kutumia mfumo uliokuwa unatumika hapo awali ambao ni njia ya simu ya mkononi na benki baada ya kupata namba ya kulipia malipo *(Control Number)* mpaka hapo watakapoingiziwa umeme.

Wamiliki wa majengo na wananchi kwa ujumla watakaokatwa kodi hiyo kimakosa na wale watakuwa na malalamiko mbalimbali, watatakiwa kufika katika ofisi za TRA zilizo karibu na maeneo yao kwa ajili ya kushughulikiwa.

Ikumbukwe kwamba, Kodi ya Majengo ilikuwa ikikusanywa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ambapo mwaka 2016/17 jukumu hili lilihamishiwa TRA na hadi sasa inaendelea kusimamia jukumu hilo.

Kwa maelezo zaidi, tafadhali wasiliana na TRA kwa kupiga simu bure toll free) kupitia namba **0800750075** au **0800780078** au barua pepe **huduma@tra.go.tz** au tuma ujumbe kwa njia ya WhatsApp kwa namba **0744 233 333.**

**Imetolewa na:**

**A. J. Kidata**
**Kamishna Mkuu**
**MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA**

216414402

# Kampuni kuzalisha mbolea kwa kutumia gesi asilia

**Na Joseph Mwendapole**

KAMPUNI ya Elsewedy Electrics ya Misri imeahidi kujenga kiwanda kikubwa cha kuzalisha mbolea kwa kutumia gesi asilia hali itakayopunguza utegemezi wa kuagiza bidhaa hiyo nje ya nchi.

Hayo yalisemwa jana na Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Uwekezaji, Godfrey Mwambe, wakati alipokuwa akizungumzia ziara yake nchini Misri na uwekezaji huo mkubwa uliopangwa kufanywa na kampuni hiyo inayojihusisha na masuala ya umeme.

Kampuni ya Elsewedy Electrics ndiyo imepata kandarasi ya kuweka umeme kwenye bwawa la kuzalisha umeme la Julius Nyerere Rufiji Mkoa wa Pwani litakalozalisha megawati 215, ambalo ujenzi wake umeshafikia asilimia 54.

Waziri alisema wizara yake na ile ya Nishati na Madini zinaendelea na mchakato wa kuangalia namna ya kuwauzia gesi hiyo ili waweze kuanza uzalishaji wanaotaka kuufanya mapema.

"Wataalamu wetu wanaendelea kukutana nao ili kuona namna ya kukamilisha mpango huu ukizingatia tunashida sana ya mbolea, watatumia gesi asilia kutengeneza mbolea aina ya amonia na baadaye urea na baadaye tutapata aina mbalimbali za mbolea," alisema Waziri Mwambe.

Alisema kuanza kwa uzalishaji wa mbolea kwenye kiwanda hicho kutasaidia sana wakulima wa Tanzania na kuziba pengo la upungufu wa mbolea ambayo imekuwa ikiagizwa nje ya nchi hivyo kuokoa fedha za kigeni na kuongeza wigo wa ajira.

"Na sasa hivi tumesikia kwamba huko duniani bei ya mbolea imeongezeka kwa hiyo tukizalisha tutauza kwenye soko ambalo bei yake ni kubwa na kupata fedha nyingi," alisema.

Mwambe alisema eneo lingine ambalo wawekezaji hao wameahidi kuwekeza ni ujenzi wa kongani ya viwanda ambalo litakuwa na ukubwa wa mita za mraba milioni mbili lenye uwezo wa kuweka zaidi ya viwanda 50 kwenye sehemu moja.

Mwambe alisema Rais Samia Suluhu Hassan alisema ni vizuri kuwa na maeneo ambayo yameshaandaliwa kwa wawekezaji kama sehemu ya kuwavutia kuja kuwekeza badala ya kuwaonyesha mapori wanapokuja kuwekeza.

Waziri alisema miezi miwili iliyopita alifanya ziara Misri ambako kulikuwa na kongamano kubwa la uwekezaji lililowakutanisha mawaziri wa uwekezaji na wakuu wa taasisi za kuhamasisha uwekezaji.

Alisema akiwa huko ambako alitumwa na Rais Samia Suluhu Hassan alihamasisha wenye viwanda jijini Cairo waje kuwekeza hapa nchini na alitembelea baadhi ya viwanda vya kule ambapo alishuhudia kongani za viwanda zinazomilikiwa na watu binafsi.



Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla (kulia), akipokea Mwenge wa Uhuru kutoka kwa Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge, katika Uwanja wa Ndege wa Julius Nyerere, kwa ajili ya kuanza kuukimbiza mkoani humo jana. **PICHA: MAULID MBAGA**

# Bunge laitaka serikali kulipa mabilioni ya MSD

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KAMATI ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC), imeitaka serikali kulipa deni la Bohari Kuu ya Dawa (MSD) Sh. bilioni 269 kwa kuwa linazorotesha ufanisi wake.

Aidha, imempongeza Mkurugenzi Mkuu wa MSD, Brigedia Jenerali, Dk. Gabriel Mhidize, kwa kufanya mabadiliko makubwa yenye tija kwa muda mfupi.

Akizungumza na Nipashe, Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Naghenjwa Kaboyoka, alisema Ofisi ya Hazina inapaswa kuhakikisha madeni ya MSD yanalipwa ili wasijue taasisi hiyo.

"Wasipolipa wanaifanya MSD ishindwe kufanya kazi, mwanzo nadhani waliacha kuwapa fedha kwa sababu kulikuwa na udanganyifu mkubwa, lakini katika bajeti ya mwaka huu wamesema wataanza kupunguza deni, tumesisitiza ili shirika hili lifanye kazi vizuri na kwa ufanisi deni lilipwe," alisema.

Alisema hatua ya MSD kuanzisha viwanda vya kutengeneza gloves, barakoa, dawa na kufufua kiwanda cha Keko ambavyo vitazalisha ajira na kuiepusha nchi kuingia kwenye madhara makubwa.

"Maana tulikuwa tunatoa gloves kutoka nje ya nchi, na malighafi ya kutengenezea gloves inatoka Zanzibar kwa kutumia miti ya mpira ambayo kwa Zanzibar ilikuwa imekaa haitumiki," alisema.

Aliutaka uongozi wa MSD kuendelea kutekeleza mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), na kwamba kamati hiyo itatembelea viwanda hivyo.

Kaboyoka aliisisitiza MSD kuendelea kuzingatia sheria za manunuzi na kufuata maagizo ya CAG.

Kwa upande wake, Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Japhet Hasunga, alisisitiza ufuatiliaji wa deni la serikali ambalo MSD inaidai kwa kuwa linaathiri afya ya taasisi.

Alisema Mkurugenzi wa MSD amefanya kazi kubwa ya kuondoa mapungufu ambayo yalikuwapo awali.

"Ameanza kujenga viwanda ambavyo ni muhimu sana kwa maendeleo ya nchi, viwanda vya dawa, gloves, barakoa, mashine za X-ray ananunua moja kwa moja badala ya kununua kwa wakandarasi ambao ni matapeli, bidhaa mbalimbali badala ya kununua kwa bei ya zabuni sasa ananunua moja kwa moja kutoka viwandani," alisema.

Alisisitiza MSD iendelee na mabadiliko mbalimbali na kuwachukulia hatua ambao wameendelea kukiuka taratibu za kiutumishi na kiutendaji na kushiriki katika ubadhirifu wa mali za umma.

# Mtendaji kijiji matatani tuhuma kuhujumu mradi

**Na Grace Mwakalinga,** KYELA

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, ametoa saa 24 kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kyela, Ezekiel Magehema, kumwandikia barua ya kumsimamisha kazi Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Mababu, Faudhia Mbilinyi.

Mtendaji huyo anatuhumiwa kushiriki kuhujumu miundombinu ya mradi wa maji katika kijiji hicho.

Katika maagizo hayo, Homera pia ametaka Mwenyekiti wa Kijiji cha Mababu, Yahaya Nsusa, naye achukuliwe hatua za kinidhamu akihusishwa na hujuma hizo.

Homera alitoa maagizo hayo jana baada ya kutembelea mradi huo na kupewa taarifa kuwa viongozi hao walishiriki katika upotevu wa mabomba yaliyopelekwa kijijini hapo kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo.

"Haiwezekani mtumishi wa serikali ashiriki katika hujuma za mali za umma ambazo zimepatikana kwa kutumia kodi ya wananchi, nakuagiza Mkurugenzi ndani ya saa 24 uwe umeshamuandikia barua ya kumsimamisha kazi ofisa mpaka kesi yake itakapokuwa imemalizika," alisema Homera.

Alisema akiwa msimamizi wa shughuli za serikali mkoani hapa, hawezi kuvumilia kuona baadhi ya viongozi wakishiriki kurudisha nyuma maendeleo ya wananchi na badala yake anahitaji viongozi washirikiane na wananchi kuleta maendeleo.

Awali, Mkuu wa Wilaya ya Kyela, Ismail Mlawa, alisema aliporipoti wilayani hapa, baada ya kuteuliwa na Rais, alifika kijijini hapo na kukuta malalamiko ya wananchi kuhusu hujuma zilizofanywa na viongozi wa kijiji hicho kwenye miundombinu ya maji.

Alisema aliambiwa na wananchi kuwa mambomba saba yaliyoletwa na Serikali kwa ajili ya ujenzi wa mradi wa maji kwenye kijiji cha Mababu yalipotea katika mazingira ya kutatanisha yakiwa mikononi mwa viongozi hao.

Mlawa alisema alipopata taarifa hizo, alimwagiza Mkuu wa Polisi Wilaya ya Kyela kuwakamata viongozi hao na kuwafikisha mahakani sambamba na kumwandikia barua Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo amchukulie hatua za kinidhamu ofisa mtendaji huyo.

Alisema polisi walitekeleza agizo lake la kuwakamata viongozi hao, lakini Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kyela alikuwa bado hajamchukulia hatua za kinidhamu ofisa huyo.

HABARI KITAIFA

## Sendiga awapa polisi siku tano

**Na Francis Godwin,** IRINGA

MKUU wa Mkoa wa Iringa, Queen Sendiga, ametoa siku tano kwa Jeshi la Polisi kuhakikisha linakamilisha upelelezi wa kesi za ubakaji na ulawiti na watuhumiwa wote kufikishwa mahakamani.

Sendiga alitoa agizo hilo wakati akizungumza na wakazi wa Kijiji cha Ingingilanyi, Wilaya ya Iringa baada ya ziara yake ya kukagua miradi ya maendeleo katika Halmashauri ya Wilaya ya Iringa, na kueleza kuwa hataki kuona kesi za ulawiti na ubakaji watuhumiwa wake wakiendelea kuachwa pasipo kufikishwa mahakamani kwani kwa ucheleweshaji huo ni chanzo cha kuongezeka kwa matukio hayo.

Hivyo, aliliagiza Jeshi la Polisi kuhakikisha upelelezi wa kesi hizo zilizofikishwa katika vituo vyote vya polisi zinafanyiwa kazi haraka ili wahusika wachukuliwe hatua sitahiki.

"Nataka kuona kesi zote za ubakaji na ulawiti watuhumiwa wake wanafikishwa mahakamani na sheria ipo wazi ubakaji na ulawiti hukumu yake ni miaka 30, hivyo niwatake wanaojihusisha na vitendo vya ukatili kama huu kutambua kuwa wakifikishwa mbele ya vyombo vya sheria adhabu ipo wazi bora tu ushahidi ukamilike," alisema.

## Waagiza upimaji wa viwanja miji 13

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

BARAZA la Madiwani la Halmashauri ya Ushetu mkoani Shinyanga, limeagiza idara ya ardhi kupima viwanja katika miji 13 inayokua ili kuondoa ujenzi holela wa makazi.

Miji hiyo ni Bulungwa, Ulowa, Nyamilangano, Ushetu, Sabasabini, Mwabomba, Nyankende, Chambo, Bugomba"B", Bugomba" A" ,Mpunze, Iboja pamoja na Ilamba.

Diwani wa Bukomela, Kulwa Shoto aliyabainisha hayo wakati wa kikao cha baraza la madiwani.

Alisema miji hiyo inakua kwa kasi na wananchi wanaendelea kujenga makazi ya kudumu bila kupimiwa viwanja vyao.

Aliongeza kuwa wananchi wa miji hiyo wamejenga makazi ya kudumu zikiwamo nyumba za biashara na kuziba sehemu zote za kupitisha gari la zima moto pale linapotokea janga la moto.

Diwani wa Sabasabini, Emmanuel Makashi, alisema miji ya Ulowa na Bulungwa wananchi wamejenga kiholela, hivyo wakati wa kutenga maeneo ya kituo cha mabasi na soko itakuwa ngumu kwa sababu maeneo mengi yamejengwa bila mpangilio.

Diwani wa Nyankende, Doa Limbu, alisema suala la upimaji la maeneo hayo baraza liliagiza tangu mwaka wa fedha 2013/2014, hivyo alitaka kufahamu kwanini mpaka sasa maeneo hayo hajapimwa na wananchi wanaendeleo kujenga makazi ya kudumu.

Mwenyekiti wa halmashauri hiyo, Gagi Lala, aliwataka maofisa wa ardhi kushirikisha wenyeviti wa serikali za mitaa pamoja na madiwani wa maeneo hayo wakati wa upimaji ili kuepusha migogoro ya mipaka.

Akijibu hoja hizo kwa niamba ya Mkurugenzi wa halmashauri, Ofisa ardhi, Juma Ngogo, alisema suala la upimaji wa viwanja katika miji hiyo limeanza muda mrefu ila limeshindwa kukamilika kwa wakati kutokana na wananchi kushindwa kulipa gharama za upimaji.

# Moto ulivyoteketeza maduka ya w'biashara

**Na Richard Makore,** MWANZA

MOTO ulioibuka usiku umeteketeza maduka ya wafanyabiashara katika barabara ya Makongoro eneo la Nera, jijini Mwanza na kusababisha hasara kubwa.

Moto huo uliteketeza maduka yaliyokuwa yanauza mafuta, rangi za nyumba pamoja na nyavu za kutegea samaki.

Akizungumza eneo la tukio, Mwenyekiti wa mtaa huo, Aboubakary Seif, alisema moto ulianza saa 10 usiku na mpaka asubuhi ulikuwa umeteketeza jengo lote lililokuwa na maduka hayo pamoja na mali zilizokuwamo.

Alisema magari ya kuzima moto yalifika kwa wakati, lakini wakati huo jengo hilo lilikuwa limeteketea karibu nusu na muda mfupi baadaye Shirika la Umeme (TANESCO), lilikata umeme na kazi ya kuzima moto ilianza.

Mwenyekiti huyo alisema magari ya zimamoto kutoka Jiji la Mwanza, Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela pamoja na Uwanja wa Ndege, yalifika kwa wakati eneo la tukio.

Alilipongeza Jeshi la Zimamoto na Uokoaji mkoani humo kwa jitihada walizofanya za kuzima moto huo usienee katika nyumba zingine ingawa taarifa ilichelewa kutolewa na hivyo kusababisha washindwe kuokoa maduka hayo.

Mmoja wa wamiliki wa maduka hayo, Shanti Kotecha, akizungumza na Nipashe katika eneo la tukio, alisema mali zake zote ziliteketea na hakuna kitu kilichookolewa.

Akizungumzia tukio hilo, Mkuu wa Wilaya ya Nyamagana, Amina Makilagi, alisema vyombo vya uokoaji vilifika kwa wakati.

Aliwataka wananchi kutoa taarifa mapema na ushirikiano kwa vyombo, ili kusaidia kuokoa mali na nyumba inapotokea ajali ya moto.

Alisema alifika eneo hilo muda mfupi baada ya ajali hiyo kutokea na kwamba vyombo vya uokoaji vilizima moto huo na kusaidia usisambae kuleta madhara katika majengo ya jirani.



Mwakilishi wa familia ya Remtulla na Shabanali, Muhammad Shaban (wa pili kulia), akizungumza na watu wenye ulemavu baada ya kuwakabidhi msaada wa baiskeli mbili za miguu mitatu na kiti mwendo kimoja, katika Kata ya Kivukoni, jijini Dar es Salaam jana. Kulia ni Diwani wa Kata hiyo, Sharik Choughule. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# DC: Sitaki umbea ofisini kwangu

**Na Ahmed Makongo,** BUNDA

MKUU wa Wilaya ya Bunda, Joshua Nasari, amekataa majungu ofisini kwake kwa kutaka taarifa sahihi, za uwazi na ukweli na kusisitiza kila mtu afanye kazi halali.

Nasari aliyasema hayo kwenye mkutano wa hadhara ulioandaliwa na Mkuu wa Mkoa wa Mara, Ali Hapi, Mji wa Bunda.

Alisema anajua kuna watu wenye majungu na kuwaomba wananchi katika wilaya hiyo wampelekee taarifa sahihi, badala ya majungu, ili serikali izifanyie kazi na kuchukua hatua madhubuti bila kumuonea mtu yeyote.

"Mimi sitaki umbea ofisini kwangu. Watu wakalime sio uongo, watu wakavue samaki sio uongo. Fursa za uvuvi zipo, fursa ya uhifadhi zipo na fursa za kilimo zipo. Na niliwahi kumuweka ndani mwananchi mmoja (jina hakulitaja) alipoleta taarifa za uongo ofisini kwangu tena akiwa amelewa na kuleta umbea... niliita OSD wakamchukua," alisema.

Aliwataka wananchi kumpelekea taarifa sahihi na yeye akiwa Mkuu wa Wilaya na Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama, atazifanyia kazi na kuchukua hatua, lakini sio umbea.

Katika hatua nyingine, aliwataka watumishi wote kutokufanya kazi kwa mazoea ikiwa ni pamoja na kutembelea wananchi na kusikiliza kero na matatizo yao, ili wayatafutie ufumbuzi kwa muda muafaka.

Aidha, aliwataka wakurugenzi kuhakikisha mapato ya asilimia iliyotengwa kwa mujibu sheria zinawafikia walengwa ambao ni vijana asilimia 40, wanawake asilimia 40 na watu wenye ulemavu asilimia 20, ili waweze kujiinua kiuchumi.

Alihimiza halmashauri kukusanya mapato ya ndani, ili fedha hizo zitekeleze miradi mbalimbali ya maendeleo katika halmashauri zao, ili kuondoa manung'uniko kwa wananchi kwamba wanachangia fedha, lakini matokeo yake hawayaoni.

# Bunge labadili utaratibu uendeshaji vikao vyake

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

BUNGE limebadili utaratibu wa uendeshaji wa vikao vya kamati zake kutokana na uwapo wa ugonjwa wa corona nchini ikiwamo kuweka idadi ya watendaji wanaoambatana na waziri kwenye vikao kutozidi maofisa watano.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Bunge, hatua hiyo inalenga kudhibiti kuenea kwa maambukizi ya ugonjwa huo.

"Kamati 14 za Kudumu za Bunge zinakutana tarehe 16 - 29 Agosti, 2021. Vikao hivi vya Kamati vinahusisha mkusanyiko wa waheshimiwa wabunge, watumishi wa Bunge, watendaji wa serikali, waandishi wa habari na wageni wengine mbalimbali, katika kutekeleza kwa vitendo tahadhari za kiafya zinazotolewa na serikali, uongozi wa Bunge umeweka utaratibu wa uendeshaji wa vikao vya Kamati," alisema.

Alitaja hatua hizo ni kutumika kwa kumbi saba kubwa kwa ajili vikao hivyo.

"Kamati zitakutana kwa kupishana yaani, saa 3:00 asubuhi - 7:30 mchana, kamati saba na saa 8:00 mchana hadi saa 12:30 jioni, kamati saba zilizosalia," alisema.

Alisema kila kamati itafanya vikao kwa namna inayozingatia muda uliopangwa, ili kutoathiri muda wa kuanza kwa vikao vya kamati nyingine.

Vile vile, alisema wageni watakaoruhusiwa bungeni kwa kipindi hicho ni wanaofika ofisini kwa shughuli za kiofisi, waandishi wa habari waliosajiliwa kwa ajili ya kutoa habari za kibunge pamoja na wadau watakaohudhuria vikao vya kamati, kwa ajili ya kutoa maoni ambao wataelekezwa na kamati inayohusika kabla ya kikao cha kupokea maoni.




Mkuu wa Idara ya Bima, Benki ya NBC, Benjamin Nkaka (katikati) na Mkuu wa Idara ya Bima kupitia benki kutoka Kampuni ya Bima ya Sanlam Life Insurance Tanzania, Klispinana Shirima, wakizindua rasmi huduma mpya ijulikanayo 'Bima ya Afya na Maisha' inayowalenga wana familia na vikundi mbalimbali vya kijamii. Wanaoshuhudia ni Mkuu wa Mawasiliano wa NBC, David Raymond (kulia) na Mabalozi wa huduma hizo, Dina Marios (wapili kushoto) na Dk. Isaac Maro (wapili kulia). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# 'Tusiwatenge waathirika wa dawa za kulevya'

**Na Julieth Mkireri,** MKURANGA

WATANZANIA wametakiwa kuwa na ushirikiano katika kutokomeza matumizi ya dawa za kulevya kwa vijana ambao wengi wao wamekuwa waathirika.

Wito huo ulitolewa na kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa, Luteni Josephine Mwambashi, alipotembelea mradi wa mapambano dhidi ya dawa za kulevya katika Shule ya Msingi Kilimahewa Wilaya ya Mkuranga.

Baada ya kukagua mradi huo na kupata ushuhuda kutoka kwa vijana waliokuwa wakitumia dawa za kulevya, kiongozi huyo alisema ni jukumu la kila mwananchi kupinga matumizi ya dawa hizo kuokoa vijana.

Aidha, Luteni Josephine alisema hakuna sababu ya kuwatenga vijana waliokuwa wakitumia dawa za kulevya, badala yake kuwapa ushirikiano wa namna ya kuacha na kuwaelimisha kazi za kufanya.

"Tusiwatenge waathirika wa dawa za kulevya tuwape elimu waache kwa pamoja tusaidie mapambano kuwaokoa vijana nguvu kazi ya Taifa," alisema.

Aliwasisitiza wananchi kushirikiana na vyombo vya dola kwa kutoa taarifa za watu wanaotumia dawa za kulevya ili wasaidiwe kuacha mapema kabla hazijawaathiri.

Akitoa taarifa ya mradi, mmoja wa waathirika wa dawa za kulevya, Nasr Majozi, alisema Wilaya ya Mkuranga inaendelea kudhibiti matumizi ya dawa za kulevya kwa kuhakikisha kunakuwapo na huduma za kitabibu na kisaikolojia kwa waathirika wanaopelekwa kwenye vituo vya kutolea huduma za afya.

Alisema wapo vijana 34 wanaohudumiwa katika vituo vya kutolea huduma za afya, lakini vipo vikundi viwili vya ujasiriamali vya vijana walioacha matumizi ya dawa za kulevya vimeundwa.

Mkuu wa Wilaya ya Mkuranga, Hadija Nasri, alisema Mwenge wa Uhuru umekimbizwa katika miradi 15 yenye thamani ya Sh. bilioni 21.1 ambayo ni pamoja na zahanati, mapambano dhidi ya Ukimwi, maji, uwezeshaji wa watu wenye ulemavu na mradi wa bwalo la Shule ya Sekondari ya Mwinyi.

# Mwenyekiti kijiji adaiwa kuuawa kwa mapanga

**Na Said Hamdani,** LINDI

MWENYEKITI wa Serikali ya Kijiji cha Kilombero, Wilaya ya Nachingwea mkoani Lindi, Eckisevia Kalembo (35), amefariki dunia kwa madai ya kucharangwa mapanga na mkewe.

Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Lindi, Foka Dinya, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo, lakini alikataa kutaja jina la mtuhumiwa, Jeshi Polisi linaendelea kumsaka mtuhumiwa huyo.

Habari kutoka kijijini hapo zilieleza kuwa mauaji hayo yanadaiwa kufanyika Agosti 14, mwaka huu mchana nyumbani kwao.

# Benki ya NBC yasaidia shule vifaa vya ujenzi

**Na Gwamaka Alipipi**

BENKI ya Taifa ya Biashara (NBC), imetoa msaada wa mabati 240, mifuko 120 ya saruji na kilo 30 za misumari kwa Shule ya Msingi Nazareth iliyopo Wilaya ya Mbinga mkoani Ruvuma.

Lengo la msaada huo ni kuunga mkono juhudi za serikali katika kuendeleza elimu kupitia ujenzi wa madarasa, ulipokelewa na Mkurugenzi wa halmashauri ya mji huo, Grace Quintine.

Akipokea msaada huo, Quintine alishukuru benki hiyo kueleza kuwa kuna upungufu wa madarasa katika shule hiyo, wilaya inasababisha msongamano madarasani.

"Serikali pamoja na wazazi tutaongeza nguvu kwenye ujenzi wa madarasa 20 ambayo yatakamilisha lengo la kuwa na jumla ya vyumba 30 vya madarasa pamoja na ofisi," alisema Quintine.

Mkuu wa Shule ya Msingi ya Nazareth, Anitha Mbungo, alisema jitihada za ujenzi zilianza mwaka 2020 kwa ushirikiano baina ya wazazi, kamati ya shule na uongozi wa kata lakini ulikwama kukamilika ujenzi wa madarasa hayo kutokana na changamoto za kifedha.

Mkuu wa Kitengo cha Wateja Binafsi wa NBC, Elibariki Masuke, aliwasihi wanafunzi wa shule hiyo kuendelea kusoma kwa bidii na kushikilia wanayofunzwa na walimu ili kuja kuwa viongozi wakubwa nchi baadaye.


Aidha, aliwapongea wazazi na uongozi wa shule kwa jitihada za kuchangia na kuanza ujenzi wa madarasa shuleni hapo.

ama
ALHAMISI AGOSTI 19, 2021
AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 13

## Ajenda kitaifa kuwalinda vijana na VVU hii hapa



Ukurasa 14

## MAAJABU ZIWA MALIWE Limejaa dagaa wenye mayai,viboko, mamba rafiki wa watu

AUGUSTINE MASSAWE

# Bingwa watoto Muhimbili aliyeasisi mbinu ya ‘kangaroo’ iliyonusuru njiti



Dokta Massawe atakumbukwa kwa kuokoa maisha ya maelfu ya watoto njiti. **PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE.**

**Na Christina Mwakangale**

TANZANIA inashika nafasi ya 20 duniani, kwa kuwa na watoto wanaozaliwa njiti wanaofikia 213,000 kila mwaka huku 40,000 wakipoteza maisha kutokana na matatizo mbalimbali ikiwamo shida ya upumuaji. Lakini pia ina asilimia 13 ya watoto wanaozaliwa kila mwaka wakiwa na uzito pungufu ‘ njiti,’ hivyo kuongeza idadi ya vifo vya watoto wachanga hususan walio chini ya umri wa mwezi mmoja, ni kwa mujibu wa wataalam wa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH).

Mikakati ya kuokoa watoto njiti na kutumia mbinu ya kangaroo inayotumiwa na kitengo cha kulea watoto njiti cha Hospitali ya Taifa Muhimbili ikiwa ni kuiga namna ya malezi ya mnyama kangaroo, anayehifadhi mtoto wake katika mfuko wa asili uliopo nje ya tumbo na kumpa joto muda wote, haiwezi kuzisahau juhudi za daktari bingwa, Augustine Massawe.

Bingwa wa Watoto na Watoto Wachanga wa siku 0 hadi 28, katika Hospitali ya Muhimbili Dk. Massawe, amefariki mwisho mwa wiki iliyopita, lakini anakumbukwa kwa jitihada nyingi za kuokoa maisha ya njiti wa taifa hili.

“Kinamama wengi hususan ambao walipitia uzazi huu na kuwafanya kuhitaji huduma za kibingwa kutoka kwa wataalamu akiwamo Dk. Massawe, ili kuokoa maisha ya watoto wao, hawatamsahau,” anasema Brigita Neema, wakati wa ibada ya kumuaga iliyofanyika Dar es Salaam, wiki hii.

Anasema hayo kwa sababu mtoto anayezaliwa chini ya miezi tisa na uzito mdogo itampasa kutumia kangaroo nyumbani au akiwa hospitalini na kuwekewa vifaa vya upumuaji, kazi aliyoifanya Dk. Massawe kuokoa maisha.

Makala hii ni kati ya nyingi ambazo Dk. Massawe alifanya mahojiano na gazeti hili, kuzungumzia mbinu mbalimbali za kuokoa njiti na kupunguza vifo akisema , wanaozaliwa na uzito mdogo ni rahisi kupoteza maisha ndani ya dakika 10, iwapo hawatakingwa na baridi na kupata nimonia ( homa ya mapafu)

Alisema watoto 260,000 huzaliwa nchini, wakiwa na uzito pungufu kutokana na sababu mbalimbali kipindi cha ujauzito, yakiwamo maradhi. Aliyasema haya kwenye maadhimisho ya siku ya watoto njiti duniani Novemba 17, 2020.

**ALIZALIWA NJITI**

Anasema aliwapenda watoto hao kwa sababu naye alizaliwa njiti... alikumbusha :”Asilimia 20 ya kinamama wanaozaa njiti wana umri mdogo. Nimefanya kazi hapa Muhimbili kwa miaka mingi nimehudumia binti wa miaka 15 ikijifungua njiti. Nimepewa jina la babu njiti, mimi nilizaliwa njiti mama yangu aliniambia hivyo.”

Aliongeza kuwa utafiti uliofanywa mapema mwaka 2020 na Muhimbili ulionyesha kuwa mbinu ya kangaroo ilipunguza vifo vya watoto njiti kwa asilimia 25. Aidha kwa kushirikiana na Shirika la Afya Duniani (WHO), kwenye nchi tano za Tanzania, Ghana, Malawi, Nigeria na India, ilibainika kuwa mtindo huo utaokoa vifo

INAENDELEA UK.12

AFYA

# Viongozi wanapoingia stendi, mnadani kupigana vita corona

**Na Marco Maduhu, SHINYANGA**

MAAMBUKIZI ya COVID-19 yalianzia China katika jiji la Wuhan mwaka 2019 hayakuicha Tanzania wala Shinyanga, yamesambaa kote duniani na sasa jitihada ni pamoja na kuhamasisha kuchanjwa na kuchukua tahadhari kudhibiti maambukizo.

COVID-19 wimbi la tatu, kirusi kinachosumbua dunia kimepewa jina la 'delta' na jitihada za kupambana na virusi hivyo ni pamoja na chanjo ya Johnson & Johnson ambayo zaidi ya watu 207,391 wameshachanjwa, kwa mujibu wa Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Profesa Abel Makubi.

Profesa Makubi anasema chanjo zaidi ya dozi 1,008, 400 zimesambazwa kwenye mikoa yote Tanzania Bara, vivyo hivyo Mkoa wa Shinyanga pamoja na kuendelea na chanjo, usafi na kuelimisha jamii umuhimu wa kufuata maelekezo yanayotolewa na wataalamu wa afya unaendelea.

Viongozi akiwamo Mkuu wa Mkoa Dk. Philemon Sengati, wametembelea masoko, minada, vituo vya mabasi na kuandaa mikutano ya watumishi wa serikali, ili kuendelea kuchukua tahadhari ya kujikinga na virusi vya corona.

Mkuu wa Mkoa Dk. Sengati katika kutoa hamasa amefanya ziara kuelimisha wananchi kujikinga na maambukizi kwenye vituo vya mabasi, maeneo ambayo ni hatarishi yenye uwezekano wa kupata maambukizi kwa wingi, kutokana na mwingiliano makubwa wa watu.

Akiwa katika kituo cha mabasi mjini Shinyanga, amewataka wamiliki wa mabasi na makodakta, kuweka ndoo za kunawa mikono kwa sabuni na maji yanayotiririka milangoni ili kila abiria anayeingia anawe mikono au kupaka vitakasa mikono na kuwa salama.

"Ndugu zangu nimefika hapa kuhamasisha uchukuaji wa tahadhari kujikinga na maambukizi ya virusi vya corona awamu ya tatu, ambavyo ni hatari zaidi na hapa kwetu Shinyanga tayari tuna wagonjwa,"anasema Dk. Sengati.

"Wekeni ndoo za kunawa mikono kwa sabuni na majitiririka, kwenye milango yote ya kuingia kituoni na hata kwenye mabasi, ili kila abiria anayeingia ndani ya basi awe salama,"anaongeza Dk. Sengati.

Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko, anapofika minadani anawakumbusha wafanyabiashara na wateja umuhimu wa kujikinga, akiwa kwenye mnada wa sokoni, maeneo ambayo yana msongamano wa watu wengi anaagiza ziwekwe ndoo za majitiririka na kutopuuzia kujikinga na maambuzi.

Mboneko akiwa katika mnada wa Tinde wilayani Shinyanga, anawaonya wafanyabiashara wanaopuuza tahadhari kujikinga na corona, huku wakiendelea na biashara zao bila ya wasiwasi na kuwaagiza ziwekwe ndoo za majitiririka kila mahali na uvaaji wa barakoa uwe kipaumbele.

"Nimesikitika sana wafanyabiashara katika mnada huu, mnafanya biashara bila kujikinga na mkitoka hapa mnakwenda kuwaambukiza watoto wenu, hebu msifanye mzaha na ugonjwa huu tutakwisha jamani,"anasema Mboneko.

"Kutokana na hali ambayo nimeiona mnada wa Tinde, naagiza minada yote Shinyanga, ziwekwe ndoo za kunawa mikono kwa sabuni na majitiririka na uvaaji wa barakoa, kujikinga,"anaongeza Mboneko.

Aidha, anasema kipindi cha corona awamu zilizopita, Tanzania ilipata unafuu kutokana na wananchi kuchukua tahadhari kujikinga, na kuwataka katika wimbi la tatu wafanye vivyohivyo ili wabaki salama.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga Dk. Yudas Ndungile, anasema wimbi la tatu la corona ni hatari, na kutaja dalili zake kuwa ni mwili kuchoka, kusikia homa, viungo kuuma, kushindwa kupumua vizuri, kuharisha, na kubainisha kuwa siyo lazima mtu akohoe wala mafua kama zilivyokuwa dalili za zamani na kuwataka kuwahi hospitalini wanapoona dalili na kwamba kuna vituo vipo kwa ajili ya kuwahudumia.

Pamoja na hospitali ya rufani anawataka waripoti katika hospitali ya Kolandoto, kituo cha afya Kambarage, Tinde, Bugharama, Nyamilangano, hospitali ya Iselamagazi, na ile ya Wilaya ya Kahama.

Kaimu Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani Shinyanga, Dk. Luzila John, anaeleza kuwa katika hospitali hiyo anasema wagonjwa wa COVID-19 waliopo wanaendelea kupata matibabu, licha ya kwamba hana mamlaka ya kutoa takwimu za wagonjwa zaidi ya Rais au Waziri wa Afya.

Aidha, anaeleza kuwa kati ya wagonjwa wa corona waliopo hospitalini hapo, wapo wanaotumia oksijeni, huku wengine wanaoendelea vizuri wataruhusiwa kuondoka, huku akitoa wito kwa wananchi kuendelea kuchukua tahadhari.

"Tunashukuru wadau wanaotuchangia mitungi ya oksijeni na mpaka sasa tumeshapokea mitungi 51 na tumeshaomba kuongezewa mingine kutoka Wizara ya Afya, ili tuendelee kuboresha utoaji wa huduma kwa wagonjwa wa corona," anasema Dk. John.



Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga Dk. Philemon Sengati (kulia), akihamasisha wananchi kwenye kituo cha mabasi cha Shinyanga Mjini, kujihadhari na corona. **PICHA: MARCO MADUHU.**

### WADAU WACHANGISHANA

Sadick Kibira, Mwenyekiti wa Klabu ya Mazoezi ya Polisi Jamii Fitness Center Shinyanga, anasema wao ni wadau wa afya, wameamua kuchangishana fedha na kununua mitungi ya oksijeni 16, ili kusaidia wagonjwa wenye corona.

"Tumetoa mitungi 16 katika hospitali ya rufani Shinyanga, ambayo itasaidia wagonjwa wenye changamoto za kupumua na tunawahimiza wananchi wajikinge na corona pamoja na kufanya mazoezi," anasema Kibira.

### UTEKELEZAJI MAAGIZO

Mwenyekiti wa Mawakala Kituo cha Mabasi mjini Shinyanga Saidi Mponda, anasema suala la abiria kujikinga na maambukizi vituoni ni la muhimu, na kuahidi kuweka ndoo za kunawa, sabuni na majitiririka kila mahali ili kujikinga na maradhi hayo.

Mwekahazina wa wafanyabiashara wadogo (machinga) mkoani Shinyanga Selemani Mwarabu, anaahidi kukutana na wafanyabiashara mara kwa mara wanaofanya biashara kwenye minada, kuwahamasisha kuchukua tahadhari kujikinga na corona wanapokuwa katika biashara zao, ili wabaki salama.

"Kirusi hakichagui umri na kutoa wito kwa Watanzania kufuta ushauri wanaopewa na wataalamu wa afya dhidi ya maradhi hayo."

AUGUSTINE MASSAWE

# Bingwa watoto Muhimbili aliyeasisi mbinu ya 'kangaroo' iliyonusuru njiti

**INATOKA UK.11**

vya watoto hao kwa nchi zinazoendelea ambazo kwa kiasi kikubwa hushindwa kumudu gharama za matibabu na vifaa vya kuongeza joto wodi ya njiti 'incubators ' katika kila hospitali.

Babu Njiti, kama alivyoitwa alisema vifaa vingine vinavyohitajika kuwaokoa ni mipira ya kupumulia, oksijeni pamoja dawa za kukomaza mapafu na kwamba njia ya kangaroo haina gharama, kwa sababu mama wa mtoto njiti anaweza kutumia nguo za asili ikiwamo kitenge kwa kumbeba mtoto wake na kumpa joto.

Bingwa huyo wa watoto alisema kwa kangaroo kama mtoto anahema kwa shida anakaa na mama yake akimbeba muda wote na kumpa joto anaimarika na kuendelea vizuri kiafya na kuongeza: "Tunataka hadithi ya theluthi moja ya watoto wanaozaliwa njiti kufariki iishe. Tunahitaji sehemu ya kutunzia watoto kila hospitali, hapa Dar es Salaam wanazaliwa watoto njiti 2,000."

### SABABU WATOTO NJITI

Dokta Massawe aliwahi kuzitaja sababu kadhaa kama mjamzito kuugua malaria, shinikizo la damu, kifua kikuu (TB), kuwa na maambukizi kwenye njia ya mkojo ( UTI), kisukari, anemia, kuwa na mapacha, uzazi wa mapema na lishe duni. Lakini, mbali na hizo zipo ambazo kitaalamu alisema hazijulikani, ni nini hasa kinachotokea tumboni na kusababisha mtoto kuzaliwa kabla ya muda.

"Tanzania kinamama wengi wanazaa watoto wenye kilo tatu, wakiwa na wiki 38 ya mimba. Akizaliwa wiki 28 ujue mtoto atakuwa na kilo moja, hii ni hatari, angalau awe amezaliwa hospitali ambako watamsimamia kikamilifu ikiwa nyumbani akipata baridi anafariki," alisema Dk. Massawe.

Aliongeza kuwa njiti wana matatizo zaidi ikilinganishwa na waliotimiza siku za kuzaliwa kwa sababu mapafu yao hayafanyi kazi kikamilifu na ni rahisi kupata maambukizi, aidha alikumbusha kuwa kila mwaka watoto 260,000 huzaliwa njiti na theluthi moja taribani watoto 80,000 hufariki ndani ya saa 24.

Alisema asilimia kubwa walio na kipato kidogo wanajifungua njiti kwa sababu ya lishe duni.

### ALICHOPENDA KIFANYIKE

Alitaka elimu kwa jamii itolewe ili ifahamu suala la njiti, aliwataka kinamama waanze kliniki mwezi wa kwanza wa mimba, badala ya kusubiri hadi mimba inaanza kupevuka . Kadhalika alitaka wahudumu wa afya wawahudumie kikamilifu wajawazito, kwa kuwapa dawa na ushauri, na kinababa wawakumbushe wake zao kuwahi kliniki ili kupunguza matatizo yanayoweza kuzuilika.

Alitaka mama mjamzito apewe muda wa kupumzika na aliyejifungua njiti aongezewe muda wa kukaa na mwanae zaidi kama anafanyakazi awe na likizo ya uzazi ya miezi mingi zaidi.

AFYA



Baadhi ya vijana walioshiriki uzinduzi wa Ajenda ya Kitaifa ya kuwekeza katika afya na maendeleo kwa vijana rikabalehe. **MPIGA PICHA WETU**

# Ajenda kitaifa kuwalinda vijana na VVU ni hii hapa

**Na Sabato Kasika**

KATIKA juhudi za kukabiliana na janga la UKIMWI, serikali imetangaza mkakati uliojikita katika nguzo sita ambazo ni kuzuia maambukizi ya VVU, kutokomeza mimba za utotoni, kuzuia ukatili wa kimwili, kingono na kisaikolojia na kuboresha lishe shuleni.

Mbali na hayo, ajenda hiyo inaelekeza watoto wa kike na kiume kubaki shuleni, ili kujengewa rikabalehe ujuzi na uwezo wa kuzifikia fursa mbalimbali za kiuchumi.

Akizindua ajenda hiyo jijini Dodoma hivi karibuni, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, anasema ni katika kusaidia rika la wanaobalehe kupata fursa ya kujiendeleza kiujuzi na kiuchumi.

Waziri Mkuu anataja hatua za kutekeleza ajenda hiyo, kwa kuanzisha programu za kuwaelimisha madhara ya kuanza ngono mapema, athari za kubeba mimba udogoni, umuhimu wa kusoma na kupata elimu, ili kujitegemea.

Kwenye lishe bora serikali na jamii itawapatia chakula wanafunzi shuleni, ili wasishinde na njaa inayozorotesha afya zao. Aidha, jamii itashiriki kudhibiti mimba za utotoni, kuzuia ukatili wa kimwili na kisaikolojia, kuhakikisha watoto wanalindwa na wanasoma hadi hatua ya mwisho.

"Ajenda hii inaelekeza kutanua wigo kwa programu ya ujuzi mwepesi (soft skills) kupitia Vyuo vya Elimu ya Ufundi (VETA) na vyuo vingine vya ufundi (Post Primary Training Colleges)," anasema Majaliwa.

Katika ufafanuzi wake, anasema, hatua hiyo ni kwa ajili ya vijana wanaomaliza shule za msingi, ili kuwawezesha kupata maarifa na ujuzi na kuwawezesha kujiajiri na kuajiriwa.

"Ajenda hii haina lengo la kuanzisha afua au programu mpya zinazokinzana na programu zilizopo katika sekta nyingine, bali ni kuimarisha na kuboresha uratibu wa pamoja ili kutekeleza afua mbalimbali zinazohusu mahitaji mahsusi ya vijana wa rikabalehe katika maeneo ya kimsingi yaliyoainishwa," anasema.

Waziri mkuu analenga kuongeza wigo wa upatikanaji wa huduma ya tohara kwa vijana wa kiume ambapo takwimu mbalimbali zinaonyesha vijana wakipata huduma hii ya tohara inawasaidia kujikinga dhidi ya maambukizi ya virusi vya UKIMWI kwa asilimia 60.

**CHIMBUKO LA AJENDA**

Anasema, chimbuko la ajenda hiyo ni kutokana na kuongezeka kwa maambukizi ya VVU na mimba za utotoni kwa vijana rikabalehe, ambapo serikali imekuja na njia ya kukabiliana na tatizo hilo.

"Takwimu za Tume ya Taifa ya Kudhibiti Maambukizi ya UKIMWI (TACAIDS), ya mwaka 2019 zinaonyesha kuwa maambukizi mapya ni milioni 3.058 na kati ya hao asilimia 50 ni vijana rikabalehe, na katika hao asilimia 80 ni wasichana na iliyobakia 20 ni wanaume," anasema Waziri Mkuu.

Anaongeza kuwa takwimu za Elimu Msingi Tanzania (BEST - 2020) zinaonyesha kuwa watoto 1,135 wa shule za msingi na 5,340 wa sekondari waliacha shule kwa sababu ya mimba hadi Desemba, 2020.

Waziri Mkuu anasema, ni lazima serikali iwekeze nguvu nyingi kwa vijana rikabalehe, hasa wa kike ili kuwa na kinamama wajao wenye afya njema, na kwamba iwapo vijana hao wataendelea kujihusisha na ngono na kuathiri afya zao na masomo, hata elimu bila malipo inayotolewa na serikali haitakuwa na maana.

> **"Takwimu za Tume ya Taifa ya Kudhibiti Maambukizi ya UKIMWI (TACAIDS), ya mwaka 2019 zinaonyesha kuwa maambukizi mapya ni milioni 3.058 na kati ya hao asilimia 50 ni vijana rikabalehe, na katika hao asilimia 80 ni wasichana na iliyobakia 20 ni wanaume," anasema Waziri Mkuu.**

"Vijana wana fursa ya kupata elimu bila kikwazo, lakini jitihada hizo hazitakuwa na maana iwapo walengwa hawatahitimu masomo, kwani matarajio ya serikali ni kuona idadi ya wanafunzi wanaoingia shule na kutoka inakuwa sawa bila kuacha mwingine nyuma," anasema Waziri Mkuu.

Anaongeza kuwa, kwa mujibu wa sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012 na makadirio ya idadi ya watu ya mwaka 2020, vijana rikabalehe wenye umri kati ya 10-19 ilifikia milioni 13.206 sawa na asilimia 22.9 ya watu wote nchini wanaingia kwenye mpango huo.

"Kati ya vijana wa kiume milioni 6.597 sawa na asilimia 49.94 na wasichana milioni 6.609 sawa na asilimia 90.05, takwimu hizo zinaonyesha kuwa vijana ni kundi kubwa linalohitaji kuwekezwa katika kuhudumiwa," anasema.

**USHIRIKISHWAJI**

Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima, anawataka wadau zikiwamo wizara za kisekta kuhusika katika kulitunza na kuliangalia kwa karibu kundi la rikabalehe.

"Serikali itaendelea kuhakikisha changamoto zinazolikabili kundi hilo ikiwamo kuambukizwa magonjwa, upungufu wa taaluma na kujiajiri, matumizi ya dawa za kulevya, ukatili wa kijinsia ndoa na mimba za utotoni vinapatiwa ufumbuzi.

Akigusia ajenda hiyo ya kitaifa, Dk. anasema, imeandaliwa kwa lengo la kutatua changamoto za upatikanaji wa huduma rafiki za afya na kuondoa vikwazo vya maendeleo kwa vijana rikabalehe nchini.

"Mimba za utotoni limekuwa mwiba kwa kipindi kirefu, kwani likiwanyima wasichana wengi fursa ya kukamilisha malengo yao katika maisha, hivyo ni muhimu kushirikiana kumaliza tatizo hili," anasema.

Dk. Gwajima anasema, hali hiyo haikubaliki, kwamba ili kuitokomeza, kila mmoja kwa nafasi yake anatakiwa kuweka mikakati ya kuwawezesha watoto wa kike kumaliza masomo yao.

**VIJANA NA DAWA ZA ARV**

Vijana rikabalehe 59,781 sawa na asilimi 61, wenye umri kati ya miaka 10 hadi 19 wanaoishi na VVU wanatambua hali zao, kati yao wavulana ni 24,937 na wasichana ni 34,844 kwa mujibu wa takwimu za Mpango wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI (NACP Desemba 2020).

Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel, anatoa taarifa hiyo kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI na Dawa za Kulevya na kufafanua kuwa 59,245 kati ya vijana hao, wameanzishiwa ARV.

"Kuna mafanikio utekelezaji wa kimataifa wa kuwakinga mabinti walio katika rikabalehe dhidi ya VVU, kwani vijana 59,781 sawa na asilimia 61 wenye umri kati ya miaka 10 hadi 19 wanaoishi na VVU wanatambua hali zao. Kati yao wavulana ni 24,937 na wasichana ni 34, 844," anasema Dk. Mollel.

Pamoja na mafanikio hayo, anasema bado vijana wanakabiliwa na kiwango kikubwa cha maambukizi mapya, ikikadiriwa kuwa zaidi ya 98,000 wenye umri kati ya miaka 10 hadi 19 wanaishi na VVU.

MAZINGIRA

## MAAJABU ZIWA MALIWE

# Limejaa dagaa wenye mayai, viboko, mamba rafiki wa watu


Muonekano wa sasa wa Ziwa Maliwe.

**Na Mwandishi Wetu**

MALIWE ni ziwa pekee katika Wilaya ya Kilwa mkoani Lindi, ambalo haliko mbali na hifadhi ya Selous . Ni eneo maarufu kwa wananchi wakilisifia kutokana na rasilimali nyingi na vivutio vya kipekee .

Ziwa hilo linamilikiwa na vijiji vitatu vya Kipindimbi, Ngea na Mitole lakini kikundi cha vijana wahamasishaji wa ulinzi wa mazingira na kutunza vyama vya maji cha Maliwe Taaluma kimebeba jukumu la kulilinda.

Akizungumza na Nipashe ilipozuru ziwa hilo, Katibu Mkuu wa Kikundi cha Maliwe Taaluma, Said Mkoba, anasema utajiri uliomo ziwani ni vivutio vingi kama viboko na mamba marafiki wa binadamu.

Wapo samaki wa aina mbalimbali na kuna visiwa nane ndani yake kikiwapo kisiwa cha ndege peke yao, cha mamba na kisiwa cha viboko.

"Kuna samaki kama kambare wasio na shombo, ngolokolo perege wasio na miiba pia zipo jamii za samaki songole na mbubu ambao ni dagaa wenye mayai. Hili ni zaidi ya ziwa kuna mengi ya kujifunza hata kwa taasisi za viumbe bahari na vyuo vikuu" anasema Mkoba.

Anawasifia viboko na mamba wanaoishi humo kuwa ni tofauti na wa sehemu nyingine, hawana ugomvi na binadamu wanaweza kupiga picha nao na hata wanapowakaribia hawawashambulii.

Mkoba anasema walianza ulinzi wa kutunza eneo hilo baada ya kupata mafunzo ya ujasiriamali jamii yakihusisha utaalamu wa kusindika mafuta ya alizeti, karanga na ufuta, kuhifadhi mazingira na vyanzo vya maji pamoja na kuhamasisha utalii wa ndani, kutoka shirika la ActionAid Kilwa.

"Tumefunzwa pia jinsi ya kutumia fursa zilizopo katika maeneo yetu au vijiji vyetu. Haya yamechochea kikundi cha Maliwe Taaluma kuanzisha mradi wa kuhifadhi Ziwa Maliwe na bayoanuai iliyopo ndani yake na msitu pia," anasema.

Kupitia mafunzo ya ActionAid, mwaka 2020 waliamua kuingia kwenye uhifadhi mazingira kwa kikundi ambacho wamekisajili ndani ya wilaya hiyo na kupitia mikutano ya mduara wa vijana , walibaini changamoto kubwa inayovikabili vijiji vinavyozunguka ziwa ni uharibifu wa mazingira, anasema Mkoba.

Ni kwa sababu wananchi walikuwa wanakata miti, kuchoma mkaa, kulima na kufuga pembezoni mwa ziwa na kusababisha kina cha maji kupungua na kuathiri viboko, mamba na uvuvi kadri miaka ilivyokwenda, anaongeza.

Mbali na hilo, msitu wa Maliwe ulianza kuharibika kwa sababu ya ufugaji wa kulisha mifugo ndani ya msitu na kuharibu sehemu kubwa ya uoto wa asili ikiwa ni pamoja na kukata miti kama mipingo.

**WANYAMAPORI WAONGEZEKA**

Kaimu Katibu Mkuu Taalum, Karim Kilunda anasema kikundi cha Maliwe kina wanachama 19 kutoka vijiji vitatu vinavyozunguka ziwa na kuongeza kuwa juhudi za kulinda mazingira zilikuwa muhimu kwa sababu uchomaji moto holela ulikithiri na kukimbiza wanyama.

"Baada ya kulinda na kuhamasisha utunzaji mazingira wanyama pori kama simba, tembo, chui, swala na ndege aina mbalimbali wamerudi katika msitu huo.

"Tunaomba mafunzo ya usalama ili tuweze kujihadhari na wanyama hawa wakati wa kujikita katika shughuli za ufugaji nyuki," anasema na kuongeza kuwa kabla ya kupata mafunzo na hamasa, hali ilikuwa mbaya.

Wakulima walilima pembezoni mwa ziwa, wafugaji kuvamia malisho na maji lakini wamefanikiwa kudhibiti wavamizi na uharibifu imepunguza ndani ya msitu.

**UWEKEZAJI KIUCHUMI**

Kilunda anasema kikundi kimesaini makubaliano na vijiji vitatu ili kulinda ziwa hilo na wamepewa heka tano kwa ajili ya kujenga miundombinu ya kitalii kama kambi , 'lodge' na hoteli na pia kuweka maeneo ya usalama na ulinzi wa mazingira.

Shughuli kubwa wanayoifanya wakati huu ni kulinda ziwa na mazingira, kuandaa vitalu vya miti na kuipanda, kulitangaza kwa wadau mbalimbali, kuhamasisha utali wa ndani, kuandaa eneo la kufuga nyuki kitaalamu lenye ukubwa wa heka 50 ili kulinda msitu na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

**CHANGAMOTO ZINAZOWAKABILI**

Kulindwa anasema ingawa wameingia katika kazi ya kutunza mazingira, wengi hawana elimu ya kutosha kuhusu shughuli za uhifadhi na kuomba msaada kutoka taasisi za uhifadhi kama Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori (TAWA), Wakala wa Misitu wa Taifa (TFS), Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa na Mfuko wa Kimataifa wa Kuhifadhi Mazingira (WWF), lakini hawajafanikiwa.

Mwanachama wa Maliwe Taaluma, Fadhili Kumbenda, anaunga mkono akisema wanahitaji elimu ya mazingira kwa sababu wanahifadhi sehemu hizo kwa kutumia njia za asili, ambacho si salama zama hizi za kidijitali.

Anataja barabara na miundombinu ya kufika ziwani hapo kuwa ni changamoto kubwa na upungufu huo unasababisha watalii na watafiti kushindwa kufika katika eneo hilo.

"Tunaiomba Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa itusaidie ujenzi wa barabara kwa sababu eneo hili ni chanzo cha mapato kwake, wananchi wanaozunguka eneo na taifa pia," anasema Kumbenda.

**MAELEZO YA VIONGOZI**

Katika mazungumzo na vijana wa Talaamu wanaeeleza kuwa licha ya kuwapo kambi ya Selous eneo hilo, Ziwa Maliwe halijafikiwa na huduma za uhifadhi.

Akijibu, Mkuu wa Kambi ya Selous Kanda ya Mashariki Maguruwe, Mluta Thabiti, anaiambia Nipashe kuwa eneo hilo halijasahauliwa ila kwa mujibu wa mipaka siyo mali ya TAWA

Anaungwa mkono na Ofisa Miundombinu wa kambi hiyo, Nicas Mvogo, kuwa wanawalinda wanyama wa sehemu hiyo na wanashirikiana na vijana wa vikundi vya ulinzi.

Thabiti anaongeza kuwa waliwapa mafunzo na vifaa kama sare walinzi wa ziwa hilo kwa kutambua moyo wa kujitolea na kuitaka Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa mmiliki wa ziwa hilo kusaidia kufanikisha juhudi za vijana hao.

Aidha, vijana wa Taaluma walitaja uharibifu wa mazingira uliofanywa na kampuni za uwindaji wakisema ziliua viboko na mamba na kuchukua ngozi, lakini hakukuwa na faidi kwa wanavijiji wala halmashauri.

Thabiti anathibitisha kuwa miaka ya nyuma kampuni ya uwindaji ya ECCO Hunting Safaris ya raia wa Ufaransa, iliruhusiwa na serikali kuwinda viboko na mamba wa eneo hilo ambalo lilikuwa kitalu cha uwindaji wa kimataifa.

"Sasa hivi sivyo, limebakia kuwa eneo la uwindaji wa ndani," anasema Mkuu wa Kambi.

**VIONGOZI WA HALMASHAURI.**

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Kilwa, Abushir Mbwana, akizungumzia Ziwa Maliwe, anasema eneo hilo limekuwa likitamaniwa na wawekezaji wengi wenye mipango mingi wakiomba walitumie kama shamba la mifugo, wengine wanataka limilikiwe na mwekezaji mmoja lakini uongozi wa wilaya ulitaka liwe kama eneo la kuvua kwa utaratibu wa 'cage fishing.'

Anasema ni mbinu ya kutega samaki kwenye eneo moja na kuwavua bila kutandaza nyavu, hata hivyo uwekezaji huo haukufanyika.

"Hili eneo litaendelezwa kupitia mpango wa mtandao wa Utalii Kilwa-Selous na Mamlaka ya TAWA na vijana watahusika kikamilifu," anaahidi Mkurugenzi Mbwana.

Anasema kwa kushirikiana na Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) mpango unaandaliwa wa kuchonga barabara kufika Maliwe.


Uharibifu wa mazingira na ongezeko la magugu maji ni changamoto inayolikabili ziwa Maliwe ambalo ni chanzo cha kipato kwa wanavijiji wanaovua samaki na kuendesha maisha. **PICHA: MPIGA PICHA WETU.**





# Ushiriki wanawake kwenye uongozi waikuna TAMWA

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

CHAMA cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) kimesema Tanzania imepiga hatua katika ushiriki wa wa wanawake kwenye masuala ya uongozi hususani wa ngazi ya juu.

Mkurugenzi Mtendaji wa TAMWA, Dk. Rose Reuben, aliyasema hayo jijini hapa alipokuwa akifungua kikao kazi cha siku moja cha chama hicho kilicholenga kuboresha maudhui ya ndani ya vyumba vya habari juu ya uongozi kwa wanawake.

Alisema wanawake wana uwezo wa kuongoza wakipewa fursa sawa za uongozi. Aidha, alisema ni muhimu kubadilisha mtazamo ambao unalenga kumkandamiza mwanamke ili aonekane hawezi kushiriki kikamilifu katika uongozi, jambo ambalo si kweli.

"Ni lazima tubadilishe mitizamo iliyopo kwa jamii, na wa kuibadilisha ni sisi wenyewe, tunahitaji ile hamsini kwa hamsini, lakini tunajipima tuko wapi au tunasafari ndefu," alisema.

Akizungumzia kuhusu mradi wa 'Wanawake wanaweza wape fursa' Dk. Reuben alisema umelenga kuimarisha usawa wa kijinsia katika masuala ya uongozi na siasa.

Alisema wanatumia vyombo vya habari kuraghabisha na kuchechemua jamii ili kubadili mienendo na kukubali kuwa wanawake ni sehemu ya maendeleo.

Hata hivyo, alisema wanataka kuona kwenye uongozi usawa wa kijinsia unafika kuwa 50/50 kama lengo la kidunia.

"Na sisi Tanzania tusibaki nyuma tunaye rais mwanamke, akiongoza wakiume makamu wake awe wa kike na akiongoza wakike makamu wake awe

wa kiume," alisema Dk. Reuben.

Alibainisha katika kutekeleza mradi huo, TAMWA imefanya kazi na vyombo vya habari zikwiamo radio za kijamii 50, vituo vya televisheni, magazeti na mitandao ya kijamii.

Kwa upande wake, Ofisa Maendeleo Mkoa wa Dodoma, Honorata Rwegasira, alisema wanafuraha kufanya kazi na TAMWA, tangu mradi huo utambulishwe

umewasaidia kuwafikia watu wengi zaidi kupitia vyombo vya habari.

"Tumetengenezewa wigo wa kuungana na waandishi wa habari, tunafanya kazi kwa pamoja hicho ni kitu kikubwa sana, kufikia mtu mmoja mmoja si rahisi lakini kupitia vyombo vya habari tumefikia watu wengi zaidi," alisema.

Naye Chifu Mazengo wa pili, alisema TAMWA imefanya kazi kubwa ya kuwasaidia wanawake wengi wanaokumbana na kero mbalimbali katika jamii.

# Simbachawene afafanua vyeti vya usajili jumuiya

**Na Mwandishi Wetu,**
DODOMA

WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi, George Simbachawene, amesema mabadiliko ya hadhi ya vyeti vya usajili wa jumuiya kutoka kuwa vya kudumu na kuwa vya kuhuishwa kila baada ya miaka tano kwa sasa yatahusisha vyama vya kijamii tu badala ya taasisi za dini.

Awali, uhuwishaji huo ulioanza Agosti 16, mwaka huu, ulilenga kuhusisha taasisi za dini na jumuiya za kijamii.

Waziri Simbachawene aliyasema hayo juzi jijini hapa katika kikao chake na Viongozi wa Mabaraza ya Kidini na mashirikisho ya dini mbalimbali nchini.

Alisema kwa sasa litahusisha vyama vya kijamii 8,851 pekee hadi hapo serikali itakapoamua vinginevyo.

"Jumla ya vyama vya kijamii 8,851 ndivyo vitakavyohusishwa katika zoezi linaloendelea hivi sasa, kupitia Ofisi ya Msajili wa Jumuiya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi," alisema.

Kwa upande wake, Msajili wa Jumuiya, Emmanuel Kihampa, alisema kufuatia mabadiliko hayo, vyama vyote vya kijamii nchini vinaagizwa kufika katika Ofisi ya Msajili wa Jumuiya iliyopo Ghorofa ya 11 katika Jengo la Kambarage jijini Dodoma, kwa lengo la kuhuisha usajili wake na kupatiwa vyeti vipya vya usajili.

Naye Mwenyekiti wa Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA), Shehe Hamis Mataka, alimshukuru waziri pamoja na uongozi wa wizara kwa kukutana na viongozi wa dini katika mkutano huo.

"Leo tunafuraha, waziri upo, Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na msajili wetu, hii inatusaidia hata migogoro mbalimbali yakidini inayokusumbua mheshimiwa waziri kwa kukutana huku kunakusaidia endapo itatengenezewa njia kupitia kukutana katika umoja huu," alisema.




Mkurungenzi wa Huduma za Kiufundi wa Shirika la Walter Aid Tanzania, Mhandisi Gloria Kafuria, akizungumza wakati wa kufungua kikao cha pamoja kati ya viongozi wa Kijiji cha Matuli, na wataalamu wa maji serikalini, jijini Dodoma juzi, kwa ajili ya ufafanuzi wa mradi wa uchimbaji kisima cha majisafi chenye thamani ya Sh. milioni 231, kitakachochimbwa na shirika hilo, kijijini hapo. **PICHA IBRAHIM JOSEPH**

# Ndachi yapata ukombozi wa maji

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

SHIRIKA la Water Aid Tanzania limewakomboa wananchi wa eneo la Ndachi jijini Dodoma na adha ya kuchangia maji ya kunywa na mifugo.

Mkurugenzi wa huduma za kiufundi wa shirika hilo, Mhandisi Gloria Kafuria, aliyasema hayo kwenye uzinduzi wa mradi huo wa maji.

Alisema shirika hilo linategemea kuanza kuchimba kisima kwa ajili ya wananchi wa eneo hilo na maeneo jirani.

Mhandisi Kafuria alisema utekelezaji wa upatikanaji wa majisafi na salama utagharimu takribani Sh. milioni 231 na unatekelezwa kwa udhamini wa Kampuni ya Serengeti Breweries Limited (SBL).

Alibainisha kuwa mradi huo ulianza kazi rasmi Julai 2021 na unalenga kukamilika ifikapo juni 2022 na lengo ni kuwafikia wananchi zaidi ya 5,521 wanaoishi kwenye eneo hilo na la Kijiji cha Ndachi na maeneo ya jirani.

Alisema mradi huo ulianza na upembuzi na sasa upo kwenye hatua ya kuanza kuchimba kisima baada ya vikao vya kuwashirikisha viongozi na wananchi wanaoshi eneo hilo kushirikishwa.

Kadhalika, alisema WateraAid Tanzania ni Shirika la Kimataifa lenye ndoto ya kuhakikisha kuwa watu wote kila mahali wanapata maji ya uhakika na huduma za usafi zilizoboreshwa ifikapo mwaka 2030.

Kadhalika, alisema shirika hilo limeweza kushirikiana na serikali pamoja na wadau wengine kuwafikia wananchi wengi hasa wale wanaoishi maeneo ya pembezoni mwa miji pamoja na vijijini kwa huduma endelevu za maji na usafi wa mazingira.

Aliongeza kuwa Shirika hilo hapa nchini limetekeleza miradi ya maji katika Mikoa ya Dar es Salaam, Arusha, Dodoma, Zanzibar, Geita, Manyara na Singida.

Naye Mkurugenzi wa Maji kutoka Wizara ya Maji, Mhandisi Lydia Joseph, aliwataka wananchi kushiriki kwa karibu katika mradi huo pamoja na kutoa ushirikiano kwa wafadhili hao.

Mhandisi Joseph aliwataka uongozi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Jiji la Dodoma (DUWASA) kujiandaa kusambaza mtandao wa mabomba na kuwaunganishia maji mradi utakapokabidhiwa kwao.

Diwani wa Mnadani, Paul Bankiye, alisema wananchi wa eneo hilo wanakabiliwa na tatizo la majisafi na kusababisha kuchangia maji na mifugo yao.

Alisema kwa sasa wanatumia maji ya mabwawa mawili yaliopo vijiji vya Ndachi na Matuli na kulishukuru shirika hilo kwa kusikia kilio chao cha miaka mingi.





# Aliyevunjika miguu sasa aomba msaada

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

JOYCE Kimena (33) Mkazi wa Mtaa wa Sinde A jijini Mbeya, ambaye alipata ajali ya gari miaka sita iliyopita na kuvunjika miguu yote, amewaomba wasamaria wema kumsaidia matibabu.

Ameomba msaada huo kwa madai kuwa tangu wakati huo mpaka sasa hajawahi kupata matibabu ya kuridhisha kutokana na matatizo ya kiuchumi.

Kimena ambaye ni mama wa mtoto mmoja, Ribert Amani, amewaomba Watanzania kumsaidia fedha za matibabu ili kuondokana na mateso na maumivu anayoyapata kwenye miguu yake.

Akizungumza na Nipashe nyumbani kwake, Kimena alisema mwaka 2015 aligonjwa na gari maeneo ya Sinde akiwa na wenzake wawili ambao wao walipona na kumsababishia majeraha miguuni.

Baada ya ajali hiyo, alisema alipelekwa katika Hospitali ya Rufani ya Kanda Mbeya (MZRH) lakini hakupata ahueni kwa sababu ya kukosa fedha za matibabu na kwamba hadi leo anaendelea kuteseka.

"Nawaomba Watanzania wenzangu msaada wa hali na mali ili nipate matibabu nipone nirejee kwenye majukumu yangu maana tangu 2015 nimekaa tu sina uwezo wa kufanya kitu chochote," alisema.

Kimena amekuwa akipata usaidizi kutoka kwa mwanawe mwenye umri wa miaka tisa anayesoma darasa la nne katika Shule ya Msingi Isanga.

Mbali na kuomba fedha za matibabu, pia anaomba msaada wa chakula kwa kuwa hivi sasa anategemea majira na wasamaria wema kumpatia chakula.

Aliongeza kuwa licha ya kuomba msaada wa chakula ma fedha za matibabu pia anawaomba wananchi kumsaidia kukamilisha ujenzi wa nyumba ambayo tayari wameanza kumjengea.

Amani aliliambia Nipashe kuwa wakati mwingine hulazimika kuahirisha masomo ili kumsaidia mama yake kazi za nyumbani ikiwamo kumwendesha kwenye baiskeli yake.

Licha ya kumhudumia mama yake pia amewaomba Watanzania kumsaidia sare za shule, madaftari na begi la shule ili aendelee kusoma kwa furaha.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Sinde A, Anyandwile Mwasanu, alisema Kimena ni yatima hana baba wala mama na kwamba anahitaji msaada wa chakula na matibabu ili aishi.

Alisema yeye amekuwa mtu wa karibu na familia ya Kimena kwa kumpatia chochote anachokipata ili asife njaa pamoja na mwanawe.



Mkazi wa Mtaa wa Sinde A, jijini Mbeya, Joyce Kimena, ambaye alipata ajali ya kugongwa na gari na kumsababishia ulemavu wa miguu tangu mwaka 2015, akipata usaidizi wa kuendeshwa kwenye baiskeli yenye magurudumu mawili na mwanae Ribert Amani (9), nyumbani kwake jana. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Wanufaika TASAF wapatiwa maarifa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

Na Grace Mwakalinga, KYELA

WANUFAIKA wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) wameshauriwa kuanza miradi mbalimbali ya ujasiriamali ili iwasaidie kujikimu kimaisha badala ya kutegemea fedha zinazotolewa na mfuko huo ambazo muda mwingine huchelewa kuwafikia.

Mwakilishi wa Mkurugenzi Mtendaji wa TASAF, Lucy Octavian, alisema hayo wakati akizunguza na Nipashe huku akisema lengo la mfuko huo ni kuwawezesha wananchi kuondokana na umaskini, hivyo fedha wanazopewa waanzishe miradi ya kujikwamua kiuchumi.

Octavian alisema kwa sasa TASAF sehemu ya pili awamu ya tatu imelenga kuwafikia wananchi wote maskini na kwamba walengwa wote lazima wafikiwe.

"Muundo wa kipindi hiki cha pili cha awamu ya tatu ya TASAF, umezingatia vyema vikwazo ambavyo vilijitokeza katika utekelezaji wa kipindi cha kwanza, hivyo kuja na maboresho zaidi.

"Nawaomba viongozi mhakikishe walengwa wanapata kila msaada unaohitajika ili kuwakwamua wananchi kiuchumi. Jambo la msingi ni kuimarisha ufuatiliaji kwenye ngazi zote kuanzia mkoa, halmashauri, kata mpaka kwenye ngazi ya jamii kufuatilia shughuli za uzalishaji mali ikiwamo ufugaji na kilimo," alisema Octavian.

Aliongeza kuwa kipindi cha kwanza cha awamu ya tatu, TASAF haikufika kwenye maeneo yote na kuibua malalamiko kwa wananchi wakihitaji kuingia kwenye mpango huo.

Mkuu wa Wilaya ya Kyela, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Magereza (SACP) Ismail Mlawa, alisema atahakikisha watendaji wanawafikia walengwa wote wa mpango huo.

Aliwataka watendaji kuzingatia kanuni na maadili kwa kuhakikisha wanawasajili walengwa wote wenye sifa za kuingizwa kwenye mpango huo.

# Wachangishana fedha kujenga maabara

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

WANANCHI wa Kata ya Sangambi katika Wilaya ya Chunya mkoani Mbeya, wamechangishana zaidi ya Sh. milioni 108 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vitatu vya maabara kwenye Shule ya Sekondari ya Kata ili kuongeza ari ya wanafunzi kujifunza masomo ya sayansi.

Mkuu wa Shule hiyo, Elly Kaminyoghe, aliyasema hayo juzi wakati wa ziara ya Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa wa Mbeya na Kamati ya Siasa ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) iliyolenga kukagua maendeleo ya mradi huo.

Mwalimu Kaminyonghe alisema mpaka kufikia Juni, mwaka jana, maboma ya vyumba vyote vitatu vya maabara yalikuwa yamekamilika na ilibakia umaliziaji na kwamba maboma hayo yalijengwa kwa kutumia nguvu za wananchi.

Alisema Machi, mwaka huu, shule hiyo ilipokea Sh. milioni 90 kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Chunya kwa ajili ya ukamilishaji wa maabara hizo.

"Mpaka sasa vyumba hivi vimekamilika na sasa hivi kinachofanyika ni kukamilisha mifumo ya umeme ambayo fundi anaendelea na kazi. Baada ya kukamilisha, wanafunzi wataendelea kuvitumia kusomea," alisema Kaminyoghe.

Diwani wa Sangambi, Junjuru Mhewa, aliishukuru serikali kwa kutoa fedha za kukamilishia jengo hilo huku akisema litawasaidia wanafunzi kusoma masomo ya sayansi.

Alisema awali shule hiyo haikuwapo na hivyo watoto wa shule hiyo walikuwa wanalazimika kusafiri umbali wa zaidi ya kilomita 20 kwenda kusoma shule zilizopo katika kata mbili za jirani ambazo ni Chalangwa na Mbugani.

Alisema mbali na fedha za ujenzi wa maabara hizo pia serikali ilitoa Sh. milioni 40 kwa ajili ya ujenzi wa Shule ya Msingi Shoga, Sh. milioni 25 kwa ajili ya Shule ya Msingi Kuliga na Sh. milioni 2.5 kwa ajili ya Shule ya Msingi Majengo Two.

"Nawashukuru sana wananchi wa kata hii wamekuwa wakijitolea sana. Mpaka sasa jengo hili limejengwa kwa ushirikiano kati ya serikali na wananchi. Lakini hawa wananchi wameendelea kujitolea kujenga kituo cha afya na miradi mingine ya maendeleo," alisema Mhewa.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alimpongeza mkuu wa shule hiyo pamoja na diwani kwa kusimamia vizuri ujenzi wa mradi huo na miradi mingine ya maendeleo inayojengwa kwenye kata hiyo.

Aliagiza shughuli zote za ukamilishaji wa maabara hizo kukamilika kabla ya Septemba 5, mwaka huu, ili ikiwezekana Mwenge wa Uhuru ukazindue na wananchi waendelee kuvitumia kujifunza kwa vitendo.

Homera pia aliwapongeza wananchi wananchi wa kata hiyo kwa kujitolea kujenga maabara hizo akidai kuwa katika baadhi ya maeneo kwenye Mkoa huo wananchi wamekuwa wavivu kujitolea kwenye shughuli za maendeleo.



## Wataka mgogoro na JWTZ upate suluhu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

WAKAZI wa Shehia ya Kikungwi, wameiomba serikali kuupatia ufumbuzi mgogoro uliopo kati yao na Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ).

Wakizungumza jana na uongozi wa serikali ya mkoa wa Kusini Unguja kwenye kikao cha kusilikiza kero za wananchi katika Shule ya Kikungwi, wananchi hao walisema mgogoro huo upo kwa zaidi ya miaka 20
sasa na bado haujapatiwa ufumbuzi.

Ali Hassan Makame, mmoja wa wananchi wa kijiji hicho, alisema mgogoro huo uliodumu kwa muda mrefu, umesababisha washindwe kuendelea na shughuli zao za kimaisha zikiwamo ujenzi na kilimo.

"Tunashindwa kufanya shughuli zetu za kiuchumi ikiwamo kilimo. Tunaiomba Serikali kuutafutia ufumbuzi mgogoro huu, tumeshachoka," alisema.

Aidha, alisema licha ya mgogoro wa ardhi pia wanakabiliwa na ukosefu wa maji safi na salama, uchakavu wa barabara ya ndani na kupanda kwa gharama za bei za bidhaa hasa vyakula hali inayosababisha kuumiza wananchi wenye kipato cha chini.

Salma Muhamed, mkazi wa kijiji hicho, alisema wizi wa mazao umekithiri kijijini hapo hali ambayo inarudisha nyuma juhudi zao za kilimo.

"Tunajitahidi kulima ili tupate chakula lakini wizi wanatuathiri kwa kutuibia mazao yetu hatuna tunachokivuna," alisema.

Akitoa ufafanuzi kuhusu mgogoro huo, Katibu Tawala wa Mkoa wa Kusini Unguja, Salum Kassim Ali, alisema serikali tayari imeshaunda tume maalum ya kushughulikia migogoro yote inayohusiana na jeshi na wananchi na tayari imeshaanza kazi ya kupitia mipaka ya asili ili kuona ufumbuzi unapatikana na
haki inatendeka kwa pande zote.

Naye Mrakibu Msaidizi wa Polisi Wilaya ya Kati Unguja, Mfaume Mohamed Mussa, akizungumzia suala la kukithiri kwa wizi wa mazao na mifugo ndani ya maeneo mbalimbali ya wilaya hiyo, aliwashauri wakazi hao kuimarisha vikundi shirikishi jamii ili kudhibiti tatizo hilo.

# Waziri Mkuya ahimiza malezi bora watoto ustawi wa taifa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Dk. Saada Mkuya Salum, amewataka wazazi na walezi kuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha watoto wanapata malezi bora ili kuwajenga katika msingi wa maadili mema.

Akizungumza jana na wanafunzi na wajumbe katika kongamano la Tuongee Faraja Club (TFC) lilioandaliwa na walimu na wanafunzi wa Shule ya Faraja katika ukumbi wa shule hiyo, alisema wazazi wasiridhike na matokeo wanayopata watoto shuleni bali wafuatilie na mienendo yao.

Alisema uanzishwaji wa klabu hiyo utasaidia kushajihisha wanafunzi kuwa na maadili mema ambayo ndio msingi wa maendeleo ya jamii pamoja na kusaidia kupunguza vitendo vya udhalilishaji.

"Vitendo vya udhalilishaji ni vingi katika jamii yetu, hivyo ni vyema tukiwa mstari wa mbele kuwalea watoto katika maadili mema pamoja na kupingana na ukatili huu. Nawapongeza walimu na wanafunzi kwa kuanzisha klabu hii ambayo ina lengo la kupinga vitendo vya udhalilishaji," alisema Saada.

Aidha, aliwashauri wanafunzi wa shule hiyo kuwa watiifu kwa walimu wao na kuiendeleza klabu hiyo yenye lengo la kuisaidia serikali katika kupinga na vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa kijinsi.

Mkurugenzi wa Udhibiti na Uchunguzi wa Tume ya Dawa za Kulevya, Juma Abdul-rahman Zidikheiry , aliitaka jamii ijiepushe na matumizi ya dawa za kulevya ili kuilinda nguvu kazi ya taifa.

Pia alisema serikali inaendelea kupanga sheria madhubuti ya kudhibiti dawa za kulevya ili kutokomeza uhalifu huo na kwamba ni kosa kujihusisa na ushiriki wa aina yoyote ikiwa kwa kuvuta, kuuza, kununua na kutumia.

Kuhusu maambukizi ya virusi vya

UKIMWI (VVU) Mwakilishi wa Tume ya UKIMWI, Halima Ali Mohamed, alisema vijana wengi kuanzia umri wa miaka 15 hadi 35 wamekuwa waathirika wakubwa wa maradhi hayo kutokana na kujihusisha na uasherati katika umri mdogo. Alisema kushamiri kwa vitendo vya ulawiti, matumizi ya dawa za kulevya na mporomoko wa maadili, kunachangia kwa kiasi kikubwa katika kusababisha maambukizi ya VVU.

Aliwashauri wazazi na walezi pamoja na walimu kuwa karibu na wanafunzi ili kutatua changamoto zinazowakabili wanapokuwa nje ya mazingira ya nyumbani au Shule ili kuepusha uwezekano wa kupata magonjwa, ikiwamo UKIMWI.



Kiongozi Mkuu wa chama cha ACT - Wazalendo, Zitto Kabwe, akizungumza katika mkutano wa majumuisho ya ziara ya chama hicho, Mjini Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Jela miaka 80 udhalilishaji, ubakaji

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

KINANA Mussa Nasibu (21) mkaazi wa Kiboje, Wilaya ya Kati Unguja, amehukumiwa kifungo cha miaka 80 jela kutokana na makosa manne ya udhalilishaji wa kijinsia ikiwamo ubakaji.

Mshtakiwa huyo alipewa hukumu hiyo jana katika Mahakama ya Mkoa wa Kusini, Mwera, na Hakimu Said Hemed Khalfan baada ya mahakama kuridhika na ushahidi uliotolewa.

Kwa mujibu wa hati ya mashtaka, Mwendesha Mashtaka wa Serikali, Shumbana Mbwana, alidai kuwa mshtakiwa huyo alitenda makosa ya udhalilishaji, kubaka na kutorosha Oktoba 18, 2019 kwa kumbaka mtoto wa miaka 15.

Pia mshtakiwa huyo alidaiwa alitenda tena makosa mengine mawili ya kutorosha na kumbaka mtoto huyo huyo ambae yuko chini ya ungalizi wa wazazi wake Novemba 2, 2019 huko Kiboje na kesi yake ilianza kufunguliwa mahakamani hapo Septemba 3, mwaka jana.

Aidha, kesi hiyo ilianza kusikilizwa ushahidi Machi 17, mwaka huu, baada ya mshtakiwa kukamatwa Tanzania Bara ambako alikimbia baada ya kufanya udhalilishaji huo.

Hakimu Said, akisoma hukumu hiyo, alisema makosa mawili ya kubaka kila kosa atumikie kifungo cha miaka 30 jela na kwa makosa mawili ya ubakaji, itakua miaka 60 na makosa mawili ya kutorosha atumikie kifungo cha miaka 20 na jumla anafungwa miaka 80.

Pamoja na hukumu hiyo, pia ametakiwa kumlipa fidia ya Sh. milioni tatu mtoto aliyedhalilishwa ili kuwa fundisho kwa watu wengine wenye tabia kama hiyo.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0782253676

## KUPOTEA KWA CHETI



**GRACE OMBENI ABRAHAM** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.0265/0009/2018** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary **CORNELIUS** mwaka **2018,** yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochite cha polisi. Polisi taarifa **MDL/K/B.I/VOL.1/107**

116413602

## KUPOTEA KWA CHETI



Ndugu **JACKSON WATSON MLAY** mwenye picha hapo juu anatangaza kupotelewa na cheti chake cha kumaliza kidato cha sita(Advanced certificate of secondary Education) chenye registration namba **S1268-0545** mwaka **2016** alichogaiwa na Baraza la Mtihani Kupitia shule ya **KISIMIRI SECONDARY SCHOOL**
Kwa yeyote atakae kiona au kuokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
**Rb Namba.MOR/MOR/RB/404581/2021**

116413402

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika Mahakama ya Mwanzo MJINI MOROGORO**
**Usimamizi wa Mirathi NO.228/2021**

Ombi la **SAID MUHDINI SAID** Kuteuliwa Msimamizi wa Mirathi ya Marehemu **AWADHI JUMA MOHAMED**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaalikwa kuja kuhudhuria shaurini mnamo **tarehe 03/09/2021** kabla huyo mwambaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo. Wosia wa marehemu huyo upo hapa mahakamani waweza kukaguliwa.
**Tarehe 02/08/2021**

HAKIMU MOROGORO

116413302

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**SABAS JOSEPH MARANDU** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina **BAJAJI** yenye namba za usajili **MC 920 CKB,** chasis namba **MD2B15B73KWF93887,** yeyotte atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi, Polisi taarifa **DAR/MSI/RB/404826/2021**

116413202

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**DONATILA MECKSON MCHAPE** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **ISUZU JOURNEY** yenye namba za usajili **T 673 DKK,** chasis namba **MR112D3000390, engine namba 6BG102846,** yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi Polisi taarifa **MKB/TRRB/139/2021**

116413702

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**NURU ABUBAKARI HAMISI** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya KINGLION yenye namba za usajili **MC 616 CTT.Chasis No. * LZL15P907LHL62943*.** Engine No. **KL162FMJ*201162943*** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOD/DOD/RB/398517/2021.**

116414002

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika Mahakama ya Mwanzo MJINI MOROGORO**

**Usimamizi wa Mirathi NO.250/2021**

**Ombi la SAID MAJALIWA MOHAMED Kuteuliwa Msimamizi wa Mirathi ya Marehemu MOHAMED SAID MAJALIWA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaalikwa kuja kuhudhuria shaurini mnamo tarehe 20/09/2021 kabla huyo mwambaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa marehemu huyo upo hapa mahakamani waweza kukaguliwa. Tarehe 18/08/2021

HAKIMU MOROGORO

116413302

## KUPOTEA KWA KADI ZA PIKIPIKI

**YUSUPH KASSIM KISWAMBA** anatangaza kupotelewa na kadi za pikipiki aina ya **BOXER BM 125 na BOXER BM 150** yenye namba za usajili **MC 243 CLX na MC 745 CHF,**chasis namba **MD2Z21BY2KWH96254** na **MD2BI5BYAKWC90539,** na engine namba **PF2WKH62306** na **JV2WKC41625**,yeyote atakayeziokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi Polisi taarifa **DAR/CFN/RB/404208/2021**

116414202


Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku

Kwa Habari Motomoto
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676
Nipashe MWANGA WA JAMII

KWA HABARI MOTOMOTO USIKOSE GAZETI LAKO LA NIPASHE KILA SIKU


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# SADC yaisifu Zambia mabadiliko kwa amani

**Lusaka, ZAMBIA**

WAKATI ikiwa ni mara ya tatu, Zambia kubadilishana madaraka kwa amani na upinzani tangu mwaka 1991, Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), imeipongeza nchi hiyo.

Barani Afrika, viongozi waliopo madarakani mara nyingi hushikilia madaraka kwa miongo kadhaa.

Rais wa Malawi, Lazarus Chakwera, akifungua mkutano wa viongozi wa SADC, mjini Lilongwe, alisema mwenendo wa makabidhiano ya madaraka kwa amani ambayo yameshuhudiwa eneo la ukanda huo, Zambia ikiwa mwanachama wa hivi karibuni kufanya hivyo, wanastahili sifa kimataifa.

Mkutano wa viongozi mjini Lilongwe utaangalia maendeleo yaliyopatikana katika kukuza na kuongeza ushirikiano wa kikanda kulingana na Dira ya 2050 ya SADC, ambayo inafikiria kuleta nchi zenye kipato cha kati mpaka juu, zenye viwanda na raia wake kufurahia ustawi endelevu wa uchumi, haki na uhuru.

Katibu Mtendaji wa SADC Stergomena Lawrence Tax ataondoka baada ya kuhudumu kwa miaka nane.

Botswana na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) zote zimeteua wagombea wa nafasi hiyo.

Botswana inataka Elias Mpedi Magosi kuchukua nafasi hiyo wakati DRC imemtaja Faustin Luanga Mukela kama mgombea wake wa wadhifa huo wa juu wa SADC.

Wakati wa mkutano wa 41, Rais wa Malawi Lazarus Chakwera, atachukua uenyekiti wa SADC kutoka kwa Filipe Nyusi, Rais wa Msumbiji.

DW

**Mkutano wa viongozi mjini Lilongwe utaangalia maendeleo yaliyopatikana katika kukuza na kuongeza ushirikiano wa kikanda kulingana na Dira ya 2050 ya SADC, ambayo inafikiria kuleta nchi zenye kipato cha kati mpaka juu, zenye viwanda na raia wake kufurahia ustawi endelevu wa uchumi, haki na uhuru.**




Mwanamke akiwa amebeba chakula akipita katika mtaa wa Les Cayes, nchini Haiti, ambao ulikumbwa na tetemeko la ardhi. Idadi ya vifo imefikia watu 2,000 kutoka 300 lilipotokea tukio hilo mwishoni mwa wiki iliyopita. **PICHA: XINHUA**

# Taliban na matumaini mapya kwa wanawake

**Kabul, AFGHANISTAN**

MSEMAJI wa Taliban, Zabihullah Mujahid, ameahidi usalama na haki kwa masuala yanayohusu wanawake na kwamba Afaghanistan itarajiwe kubadilika kiuchumi.

"Tunamhakikishia kila mmoja, taifa lote kila kitu kitakuwa sawa na mabadiliko yataendelea kuboreka na kuondoka katika hali iliyopo sasa."

Msemaji huyo aliyasema hayo jana mbele ya vyombo vya habari mjini Kabul, Afghanistan, kwa mara ya kwanza kujitokeza hadharani ambaye awali alitoa matamko kuhusu Taliban bila kujitokeza.

Akizungumza kwenye mkutano huo ikiwamo kujibu maswali kadhaa kutoka kwa waandishi aligusia kuhusu haki za wanawake, usalama na namna watakavyorejesha hali ya utulivu nchini humo baada ya Taliban kuchukua mamlaka.

Kwa miaka mingi, amefanya kazi nyuma ya pazia, sauti tu kupitia simu ndio ilikuwa inasikika.

"Wanawake ni watu muhimu katika jamii tunawahakikishia haki kulingana na taratibu za kiislamu. Wageni hawatakiwi kuondoka nchini"

"Kwa miaka mingi ametuma ujumbe wa umwagaji damu na sasa ghafla, anataka amani? Ni vigumu sana kuunganisha hilo".

"Haki za wanawake nchini Afghanistan zitaheshimiwa kulingana na mfumo wa sheria za Kiislamu", Taliban alisema.

Katika mkutano wa kwanza na waandishi wa habari tangu Taliban walipochukua udhibiti wa nchi ya Afghanistan Jumapili, msemaji alisema wanawake watakuwa huru kufanya kazi lakini akatoa maelezo kidogo juu ya sheria na masharti mengine.

Msemaji wa kundi hilo Mujahid alirudia kwamba Waafghanstan wote lazima waishi katika mfumo wa Uislamu.

Hata hivyo, vikundi vya kutetea haki vinahofia uhuru wa wanawake unaweza kukadamizwa tena chini ya Taliban.

Kundi hilo la wapiganaji liliandisha au kuunga mkono adhabu kulingana na tafsiri yao kali ya mfumo wa sheria ya Kiislam, yaani Sheria, wakati walipodhibiti Afghanistan kati ya 1996 na 2001.

Wanawake walilazimika kuvaa burka inayofunika kila mahali, na Taliban pia hawakukubali wasichana wenye umri wa miaka 10 na kuendelea kwenda shule.

Katika mkutano huo na wanahabari juzi, Mujahid alijibu maswali kadhaa kutoka kwa wanahabari wa kimataifa juu ya haki za wanawake chini ya serikali ya Taliban.

"Tutaruhusu wanawake kufanya kazi na kusoma ndani ya mifumo yetu. Wanawake watakuwa wachangamfu sana katika jamii yetu".

Lakini hakufafanua alipoulizwa juu ya kanuni za mavazi na ni majukumu gani wanawake wataweza kuwa nayo ndani ya nguvukazi ya nchi.

TRUMP AMKOSOA MRITHI WAKE

RAIS wa zamani wa Marekani, Donald Trump, alimkosoa mrithi wake Joe Biden, jinsi alivyoshughulikia suala la Afghanistan

Trump aliyasema hayo katika mahojiano na kituo cha habari cha Fox News, Marekani.

Rais huyo wa zamani wa Marekani pia alikosoa kujiondoa kwa Biden Afghanistan na vile alivyoshughulikia suala la wanaovuka mpaka wa Mexico ambayo idadi yake hivi karibuni imepita ile iliyorekodiwa kwa kipindi cha miongo miwili.

"Angalia kile alichokifanya Biden katika mpaka wa kusini... hali ilivyo nchini Afghanistan ni kama mpaka wa Kusini lakini imeshughulikiwa vibaya zaidi.

"Hakuna mtu aliyeshughulikia suala la mpaka wa kusini vibaya zaidi kuliko yeye, Afghanistan vivyo hivyo", alisema.

Trump pia alidai kwamba angeshughulikia uondoaji wa majeshi kwa njia tofauti.

"Nilipunguza jeshi la Marekani nchini Afghanistan kutoka karibu 20,000 hadi wanajeshi 2,500 na sasa wanaondoa tena wanajeshi kabla hatujatoa raia wetu na wakalimani na watu wengine ... waliotusaidia.

"Sasa basi, tulichokuwa tunatakiwa kufanya ni kuchukua wanajeshi wetu, mwisho, watu walitakiwa wawe wa kwanza kuondoka," alisema.

Wakati huo huo, Kamanda wa Taliban na kiongozi wa juu wa mtandao wa wanamgambo wa Haqqani, Anas Haqqani, amekutana na Rais wa zamani wa Afghanistan Hamid Karzai kwa mazungumzo.

Ofisa wa kundi la Taliban alisema mkutano huo umefanyika, jana, huku kukiwa na juhudi za Taliban kuunda serikali.

Ofisa huyo wa Taliban ambaye hakutaka kutajwa jina alisema Karzai aliongozana na mjumbe mkuu wa amani katika serikali iliyopita, Abdullah Abdullah, katika mkutano huo.

Mtandao wa Haqqani ni kundi muhimu la Taliban, ambao siku ya Jumapili uliudhibiti mji mkuu wa Afghanistan, Kabul.

Waziri Mkuu wa Uingereza Boris Johnson alisema nchi yake itafanya kila iwezalo kuepusha migogoro Afghanistan.

Akilihutubia jana, Johnson alielezea hali ya Taliban kudhibiti Afghanistan kuwa inayoenda kwa kasi kuliko ilivyotarajiwa.

*BBC/DW*

MECHI KALI
HOME
RANDERS
3.36 | 3.36 | 2.15
GALATASARAY
AWAY

1 WEKA PESA.
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4 - WEKA PESA.
vodacom m-pesa airtel money tigo pesa EZYPESA
- FUNGUA MENYU YA HALOPESA
- CHAGUA LIPA/LIPIA BILI
- WEKA NAMBA YA KAMPUNI 150888, KUMBUKUMBU 888.
- KISHA WEKA 500 AU ZAIDI.
SEND
halopesa

2 WEKA BET.
- PIGA *150*87#
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249
18+
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 433

# COUTINHO CHAMBO YA AUBAMEYANG



**BARCELONA, Hispania**

BARCELONA wanavutiwa na nahodha wa Arsenal, Pierre-Emerick Aubameyang na wako tayari kumtumia Philippe Coutinho kama chambo ya kumnasa, kwa mujibu wa ripoti.

Miamba hiyo ya Catalunya bado ipo kwenye wakati mgumu baada ya kuondoka kwa Lionel Messi, na Rais Joan Laporta amesema wana deni la pauni bilioni 1.15 licha ya kumtoa Muargentina huyo.


Lakini kocha Ronald Koeman bado anahitaji kujaza nafasi ya mshambuliaji iliyoachwa na Messi, na kwa mujibu wa Sky Sports, Aubameyang mwenye umri wa miaka 32, anaonekana kama usajili mzuri ingawa haiwezekani kuwa mpango wa moja kwa moja wa mshambuliaji huyo.

Klabu hiyo ya LaLiga inaripotiwa kuwa tayari kumtoa mchezaji wa zamani wa Liverpool, Coutinho kuwa sehemu ya kubadilishana ili kufanikisha uhamisho huo.

Itakuwa pigo kwa kocha, Mikel Arteta kumpoteza nahodha wake mwishoni mwa dirisha, lakini Arsenal imekuwa ikijaribu kusaini kiungo wa ubunifu na Coutinho anafaa kwa mpango huo.

Wote Aubameyang na Alexandre Lacazette walikosa mchezo wa kichapo cha mabao 2-0 siku ya ufunguzi wa Ligi Kuu England dhidi ya Brentford.

# Locatelli rasmi Juventus



**TURIN, Italia**

JUVENTUS wamefikia makubaliano ya kumsajili, Manuel Locatelli kutoka Sassuolo kwa makubaliano ya mkopo ambayo ni pamoja na kipengele cha kumnunua moja kwa moja kwa euro milioni 35, kwa mujibu wa vyombo va habari vya Italia.

Miamba hao wa Serie A wamekuwa wakifuatilia saini ya Locatelli kwa miezi mingi, baada ya kumuona akifurahia kampeni nzuri ya msimu wa 2020-21 kule Sassuolo kusaidia klabu kupata nafasi ya nane kwenye ligi.

Arsenal pia ilikuwa ikihusishwa sana na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23, lakini nafasi anayopendelea zaidi imekuwa Uwanja wa Allianz na Bianconeri hao sasa wamefanikiwa kufikia makubaliano.

Locatelli sasa atajiunga na safu ya kiungo ya nyota wote wa kocha Massimiliano Allegri kwenye Uwanja wa Allianz ambapo atakuwa akishindania dakika pamoja na wachezaji kama Federico Bernardeschi, Dejan Kulusevski, Adrien Rabiot na Aaron Ramsey.

Mchezaji huyo amethibitisha kuwa anaweza kushughulikia mahitaji ya kucheza kwa kiwango cha juu tayari, ingawa, alikuwa na jukumu muhimu katika mbio za Italia kwenye ubingwa wa Mashindano ya Ulaya mapema mwaka huu.

## HABARI MICHEZO

3,401,140

JACKPOT

MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 21/08/21 | 17:00 | Crystal Palace vs Brentford | 2.70 | 3.10 | 2.75 |
| 02. 21/08/21 | 17:00 | Leeds vs Everton | 2.22 | 3.53 | 3.12 |
| 03. 21/08/21 | 17:00 | Coventry vs Reading | 2.20 | 3.25 | 3.20 |
| 04. 21/08/21 | 17:00 | Cardiff vs Millwall | 2.24 | 3.21 | 3.16 |
| 05. 21/08/21 | 17:00 | Blackburn vs West Bromwich | 2.76 | 3.25 | 2.47 |
| 06. 21/08/21 | 18:00 | Alaves vs Mallorca | 2.47 | 3.16 | 3.01 |
| 07. 21/08/21 | 19:30 | Verona vs Sassuolo | 2.86 | 3.36 | 2.45 |
| 08. 21/08/21 | 20:30 | Granada vs Valencia | 2.49 | 3.28 | 2.87 |
| 09. 22/08/21 | 16:00 | Wolverhampton vs Tottenham | 3.42 | 3.22 | 2.21 |
| 10. 22/08/21 | 16:00 | Lokomotiv Moscow vs FC Krasnodar | 2.40 | 3.36 | 2.77 |
| 11. 22/08/21 | 16:00 | Bordeaux vs Angers | 2.80 | 3.30 | 2.48 |
| 12. 22/08/21 | 18:00 | UD Ibiza Eivissa vs Malaga | 2.73 | 2.78 | 2.87 |
| 13. 22/08/21 | 21:45 | Nice vs Marseille | 2.88 | 3.18 | 2.48 |

MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

ALHAMISI - 19 - AGOSTI 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:35 | 1710 | Suzhou Dongwu vs Chengdu Qianbao | 5.41 | 4.06 | 1.51 |
| 16:00 | 1347 | Shakhter Karagandy vs Maccabi Tel Aviv | 4.25 | 3.14 | 1.85 |
| 17:00 | 3583 | Eidsvold Turn vs Hodd | 2.95 | 3.95 | 2.14 |
| 18:00 | 1785 | Flekkeroy vs Egersund IK | 4.75 | 4.17 | 1.55 |
| 18:00 | 2558 | Metaloglobus vs Hermanstadt | 2.90 | 3.15 | 2.55 |
| 18:00 | 3519 | TPS Turku vs RoPs Rovaniemi | 1.52 | 3.83 | 5.63 |
| 18:15 | 2143 | Emirates Club vs Shabab AL Ahli Dubai Club | 7.20 | 4.80 | 1.40 |
| 19:00 | 1524 | Rakow Czestochowa vs KAA Gent | 3.43 | 3.33 | 1.99 |
| 19:00 | 2893 | OKS Odra Opole vs Zaglebie Sosnowiec | 2.36 | 3.24 | 2.76 |
| 19:00 | 3401 | Flora Tallinn vs Shamrock Rovers | 2.72 | 3.20 | 2.41 |
| 19:00 | 3735 | Karabakh vs Aberdeen | 2.32 | 3.06 | 2.96 |
| 19:00 | 3834 | Vendsyssel FF vs Horsens | 3.10 | 3.39 | 2.09 |
| 19:00 | 4665 | KuPS Kuopio vs Union Berlin | 7.94 | 5.04 | 1.30 |
| 19:00 | 4996 | Alianza Atletico vs Alianza Universidad De Huanuco | 2.32 | 3.04 | 2.99 |
| 19:00 | 5667 | KS Gornik Polkowice vs Chrobry Glogow | 2.36 | 3.19 | 2.80 |
| 19:10 | 4615 | AL Hazm vs Al Ahli Jeddah | 3.81 | 3.86 | 1.82 |
| 20:00 | 1110 | LASK Linz vs St Johnstone | 1.44 | 4.16 | 6.19 |
| 20:00 | 2689 | FC Riga vs Lincoln FC | 1.51 | 4.06 | 5.41 |
| 20:00 | 3867 | Neftchi Baku vs Maccabi Haifa | 3.14 | 3.33 | 2.10 |
| 20:00 | 4468 | Zalgiris vs Bodo Glimt | 4.15 | 3.77 | 1.70 |
| 20:00 | 4682 | Slavia Prague vs Legia Warszawa | 1.59 | 3.89 | 5.79 |
| 20:00 | 4763 | Omonia Nicosia vs Royal Antwerp | 2.76 | 3.11 | 2.66 |
| 20:00 | 5072 | Hapoel Beer Sheva vs Anorthosis Famagusta | 1.80 | 3.39 | 4.07 |
| 20:00 | 5573 | Randers vs Galatasaray | 3.36 | 3.36 | 2.15 |
| 20:00 | 5918 | Viktoria Plzen vs CSKA Sofia | 1.64 | 3.63 | 4.74 |
| 20:30 | 1056 | Ajman Club vs Al Nasr Dubai | 5.43 | 4.46 | 1.46 |
| 20:30 | 1929 | Fola vs Kairat Almaty | 3.05 | 3.24 | 2.18 |
| 20:30 | 2749 | FC Basel vs Hammarby | 1.39 | 4.45 | 6.58 |
| 20:30 | 4384 | Trabzonspor vs Roma | 3.82 | 3.43 | 1.85 |
| 20:50 | 5483 | Al Faisaly (KSA) vs Al Nasr Riyadh | 5.15 | 4.36 | 1.55 |
| 21:00 | 1422 | NK Mura vs Sturm Graz | 4.20 | 3.70 | 1.81 |
| 21:00 | 2943 | PAOK vs HNK Rijeka | 1.64 | 3.48 | 5.03 |
| 21:00 | 3040 | Sivasspor vs Copenhagen | 2.85 | 3.33 | 2.25 |
| 21:00 | 3957 | UMF Grindavik vs Throttur Reykjavik | 1.53 | 4.54 | 4.54 |
| 21:00 | 4281 | Baumit Jablonec vs MSK Zilina | 1.97 | 3.65 | 3.60 |
| 21:00 | 4531 | Rennes vs Rosenborg | 1.49 | 3.24 | 8.70 |
| 21:00 | 4737 | Anderlecht vs Vitesse Arnhem | 1.98 | 3.30 | 3.49 |
| 21:00 | 5030 | Feyenoord vs Elfsborg | 1.39 | 4.47 | 6.61 |
| 21:00 | 5281 | Afturelding vs IF Vestri | 2.27 | 3.78 | 2.57 |
| 21:30 | 1674 | GKS Katowice vs Sandecja | 2.15 | 3.20 | 3.16 |
| 21:30 | 2766 | Pacos Ferreira vs Tottenham | 5.61 | 4.16 | 1.48 |
| 21:45 | 3930 | Fenerbahce vs HJK Helsinki | 1.36 | 5.22 | 7.63 |
| 22:00 | 2215 | Olympiakos vs Slovan Bratislava | 1.43 | 4.39 | 7.59 |
| 22:00 | 2763 | Pyramids vs Aswan | 1.45 | 4.33 | 6.50 |
| 22:00 | 2890 | Rangers vs Alashkert Martuni | 1.15 | 7.58 | 17.94 |
| 22:00 | 3882 | Rapid Vienna vs Zorya Lugansk | 1.81 | 3.71 | 4.22 |
| 22:15 | 4286 | Fram Reykjavik vs UMF Selfoss | 1.38 | 5.05 | 5.83 |
| 22:15 | 4540 | Grotta vs Kordrengir | 2.31 | 3.58 | 2.61 |
| 23:30 | 2691 | Univ San Martin vs Academia Cantolao | 2.21 | 3.24 | 3.00 |
| 23:30 | 4163 | Santa Clara vs Partizan | 2.90 | 3.23 | 2.27 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# ALGERIA, IVORY COAST KUNDI MOJA AFCON 2021



CAF® TOTAL AFRICAN NATIONS CHAMPIONSHIP

**CAIRO, Misri**

BINGWA mtetezi wa michuano ya Mataifa ya Afrika, AFCON, Algeria, wamepangwa kundi moja na mabingwa wa mara mbili wa mashindano hayo, Ivory Coast katika droo ya michuano hiyo kwa mwaka 2021 iliyofanyika Yaounde nchini Cameroon, Jumanne.

Michuano hiyo iliyochelewa itafanyika nchini Cameroon kuanzia Januari 9 hadi Februari 6, mwakani, zikihusisha timu 24 na kukiwa na makundi sita.

Algeria, ambao walishinda taji hilo mwaka 2019 nchini Misri, wamepangwa na mabingwa wa mwaka 1992 na 2015, Ivory Coast pamoja na Sierra Leone na Equatorial Guinea katika Kundi E.

Waandaaji Cameroon, watafungua michuano hiyo wakiwa Kundi A, ambapo wamepangwa na Burkina Faso, Ethiopia na Cape Verde.

Bingwa mwenye rekodi ya kubeba mara saba taji hilo, Misri ambao kwa mara ya mwisho walitwaa mwaka 2010, wamepangwa Kundi D na mabingwa mara tatu, Nigeria, Sudan na Guinea-Bissau.

Wachezaji wa Arsenal, Pierre-Emerick Aubameyang na Thomas Partey watakutana kwenye Kundi C wakati timu zao za Gabon na Ghana zikipangwa pamoja na Comoros na Morocco.

Gambia ambao wamefuzu kwa mara ya kwanza wapo Kundi E pamoja na Tunisia, Mali na Mauritania, huku washindi wa pili wa mwaka 2019, Senegal wakiwa Kundi B pamoja na Zimbabwe, Guinea na Malawi.

**Makundi kamili:**

| | |
|---|---|
| **Kundi A:** | Cameroon, Burkina Faso, Ethiopia, Cape Verde |
| **Kundi B:** | Senegal, Zimbabwe, Guinea, Malawi |
| **Kundi C:** | Morocco, Ghana, Comoros, Gabon |
| **Kundi D:** | Nigeria, Misri, Sudan, Guinea-Bissau |
| **Kundi E:** | Algeria, Sierra Leone, Equatorial Guinea, Ivory Coast |
| **Kundi F:** | Tunisia, Mali, Mauritania, Gambia |




# *Laporta: Uchumi wa Barcelona dhaifu*

**BARCELONA, Hispania**

JOAN Laporta ameelezea jinsi hali ya kifedha ya Barcelona ilivyo dhaifu wakati wa mkutano na waandishi wa habari siku ya Jumatatu, ikiwa na hasara ya euro milioni 451.

**Baada ya kulinganisha hali yao na klabu nyingine, Laporta amethibitisha kuwa Barcelona imekuwa ikitumia fedha nyingi zaidi kulipa mishahara.**

"Barcelona wana jumla ya hasara ya euro milioni 451," alitangaza Laporta na pia kuwa na "muswada wa mshahara ambao unawakilisha asilimia 103 ya mapato yote ya klabu. Inawakilisha asilimia 20-25 zaidi kuliko washindani wetu."

Laporta alibainisha kuwa hawajapata urahisi kuwahimiza wachezaji kukubali mikataba ya kushuka kwa mishahara yao.

"Tumepata hali ngumu wakati wa kujadili tena mikataba ya wachezaji," aliongeza Laporta."

HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI ULAYA




# RONALDO AJA JUU MADAI KUACHANA NA JUVENTUS

● ● ● Kinachozungumzwa na vyombo vya habari kunihusisha na klabu nyingine ni kunikosea...

**TURIN,** Italia

CRISTIANO Ronaldo amezishutumu ripoti za vyombo vya habari kumhusisha yeye na mpango wa kuondoka Juventus.

Katika ujumbe aliouweka kwenye ukurasa wake wa Instagram hakuonyesha kukataa au kukubali uwezekano wa kubaki kwa miamba hao wa Italia.

Lakini mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 36, amesema kwa sasa "akili yangu ni kazi" licha ya uvumi kumhusisha na Real Madrid, Paris Saint-Germain na Manchester City.

Nahodha huyo wa Ureno ameuita uvumi huo kuwa "dharau kwangu kama mtu na kama mchezaji."

Aliongeza: "Hebu tuzungumze na tufanye kazi, hilo limekuwa mwongozo wangu tangu nilipoanza maisha ya soka.

"Hata hivyo, kila kitu kilichoandikwa na kuzungumzwa hivi karibuni, sijakizingatia kwa sasa.

"Kile kinachozungumzwa na vyombo vya habari kuhusu majaliwa yangu na kunihusisha na klabu nyingine ni kunikosea heshima."

Mapema Jumanne, kocha mpya wa Real Madrid, Carlo Ancelotti, alijibu uvumi kuhusu kumtaka Ronaldo kupitia kwenye tweeter, akikanusha kuhusishwa na kumwania Ronaldo katika klabu yake.

"Cristiano ni mchezaji gwiji wa Real Madrid na ana mapenzi na heshima zote. Sijawahi kufikiria kumsajili yeye. Tunaangalia mbele," aliandika Ancelotti.

Ancelotti alijibu uvumi huo baada ya Televisheni ya El Chiringuito ya nchini Hispania kuripoti kwamba, kumekuwa na mazungumzo kati ya Real Madrid na Ronaldo kuhusu uwezekano wa kumsajili katika klabu hiyo aliyoondoka miaka mitatu iliyopita na kutua Juventus kwa pauni milioni 99.2.

Ronaldo alijiunga na Real akitokea Manchester United Julai mwaka 2009 na alifunga mabao 450 katika mechi 438 kwa kipindi cha misimu tisa aliyokaa hapo.

## ZISIKUPITE

### ODEGAARD ANUKIA ARSENAL

UHAMISHO wa Martin Odegaard kutoka Real Madrid kwenda Arsenal unakaribia huku kukiwa na taarifa kwamba kiungo huyo wa kati mwenye umri wa miaka 22, hakushiriki mazoezi na timu ya Real, Jumanne. ***(The Athletic)***

### RONALDO APELEKWA CITY

WAKALA wa mshambuliaji wa Juventus, Cristiano Ronaldo, Jorge Mendes, amewapa Manchester City ofa ya kumsajili nyota huyo wa Ureno mwenye umri wa miaka 36. ***(Corriere dello Sport)***

### CITY BADO KWA KANE

MANCHESTER City imesisitiza kwamba, bado inamlenga zaidi mshambuliaji wa Tottenham Hotspur na England, Harry Kane mwenye umri wa miaka 28. ***(Mirror)***

### ARSENAL KUMKOSA TRIPPIER

KLABU ya Atletico Madrid imeziambia Arsenal na Manchester United kwamba, beki wa kulia wa England, Kieran Trippier mwenye umri wa miaka 30, hauzwi. ***(AS)***

### PSG BADO WAKOMAA

KLABU ya Paris St-Germain haijaondoa uwezekano wa uhamisho wa dakika za mwisho wa viungo wa kati raia wa Ufaransa Paul Pogba mwenye umri wa miaka 28 kutoka Manchester United na Eduardo Camavinga kutoka Rennes. ***(L'Equipe)***

### MBAPPE KUUZWA MADRID

PSG ina nia ya kumuuza mshambuliaji wa Ufaransa, Kylian Mbappe mwenye umri wa miaka 22, kwa Real Madrid msimu huu. ***(Mundo Deportivo)***

### ZOUMA ATAKIWA TOTTENHAM

KLABU ya Tottenham Hotspur inafikiria uhamisho wa mlinzi wa Chelsea, Kurt Zouma. Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 26, pia anahusishwa na uhamisho wa West Ham msimu huu. ***(Sky Sports)***

### RAMSDALE AWANIWA ARSENAL

ARSENAL imeanzisha tena mazungumzo na Sheffield United juu ya makubaliano ya mlinda mlango wa England, Aaron Ramsdale mwenye umri wa miaka 23. ***(The Athletic)***

### RODRIGUEZ AIKANA ATLETICO

NYOTA wa Everton, James Rodriguez amekanusha taarifa kwamba anatafuta uhamisho wa kwenda Atletico Madrid, baada ya ujumbe wa Twitter wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30 raia wa Colombia kuchukuliwa kama kidokezo kwamba anahamia kwa mabingwa hao wa LaLiga. ***(Liverpool Echo)***

### GUEDES AWINDWA WOLVES

KLABU ya Wolverhampton Wanderers inajitayarisha kutoa ofa ya pauni milioni 21 kwa Valencia ikimlenga winga wa Ureno, Goncalo Guedes mwenye umri wa miaka 24. ***(Birmingham Mail)***

### CHOUDHURY AWANIWA NEWCASTLE

KOCHA wa Newcastle, Steve Bruce anamwinda kiungo wa kati wa Leicester, Hamza Choudhury mwenye umri wa miaka 23 kwa mkopo. ***(Mail)***

## HABARI MICHEZO

### Ndayiragije, Hererimana wala shavu Ligi Kuu Bara

**Na Tunu Hassan, TUDARCo**

WAKATI uongozi wa klabu ya Mbeya Kwanza jana ukimtambulisha rasmi Haruna Hererimana kuwa kocha mkuu wa timu hiyo kuelekea msimu mpya wa 2021/22, huko Geita Gold FC nako kunaelezwa 'kimenuka' kwa aliyekuwa kocha mkuu wa timu hiyo, Felix Minziro, baada ya kocha wa zamani wa Taifa stars, Etienne Ndayiragije kutajwa kuwa mbioni kuchukua mikoba yake.

Mbeya Kwanza iliyopanda daraja msimu huu, jana ilimtangaza Hererimana kuwa kocha mkuu wa timu hiyo akichukua nafasi ya Steven Matata aliyeipandisha Ligi Kuu, hiyo ikiwa ni timu yake ya tatu kuipandisha daraja.

Hererimana ambaye ni raia wa Burundi, aliwahi kukinoa kikosi cha kmc msimu wa 2019/20 akichukua mikoba ya Jackson Mayanja na kufanikiwa kuwa kocha bora wa Machi msimu huo.

Akizungumza na Nipashe jana, Mwenyekiti wa Mbeya Kwanza, Mohamed Mashango, alisema lengo la kufanya mabadiliko hayo ni kupata kocha anayeijua Ligi ya Tanzania na kwamba Hererimana ni mtu sahihi kwao.

Kwa upande wa Ndayiragije kutua Geita Gold, chanzo chetu cha uhakika ndani ya klabu hiyo, kililieleza gazeti hili: "Ni kweli tunamchukua kocha wa zamani wa timu ya Taifa ya Tanzania 'Taifa stars', Etienne Ndayiragije, achukue mikoba ya kocha Felix Minziro

### Mgunda abadilishiwa majukumu Coastal

**Na Tunu Hassan, TUDARCo**

UONGOZI wa Coastal Union umembadilishia majukumu Kocha Mkuu wa timu hiyo, Juma Mgunda, ambapo sasa atakuwa Mkurugenzi wa Ufundi wa timu hiyo huku Mmarekani Melis Medo, akitajwa kwenda kurithi mikoba yake.

Medo anayetajwa kwenda kuchukua mikoba ya Mgunda, msimu uliopita aliinoa Gwambina FC akirithi mikoba ya Mohammed Badru wakati zikiwa zimebaki mechi chache kabla ya msimu kumalizika.

Akizungumza na mwandishi wetu jana, Mwenyekiti wa Coastal Union, Steven Mnguto, alikiri Mgunda kubadilishiwa majukumu katika kikosi hicho huku kuhusu Medo kurithi mikoba yake akishindwa kukataa ama kukubali zaidi ya kueleza kwamba muda ukifika wataweka kila kitu wazi.

Nipashe lilipomtafuta Mgunda kuhusu alivyopokea majukumu hayo mapya, alisema: "Mwenyekiti akishasema tufuate alichokisema, kwa sasa nipo Dodoma namaliza mambo yangu huku nitarudi Tanga kesho [leo]," alisema Mgunda.

# KAMPENI YA 'KAPU LA WANA' YA PILSNER LAGER YAGEUKA LULU

**Na Mwandishi Wetu**

IKIWA ni siku chache tangu kuzinduliwa kwa Kampeni ya 'Kapu La Wana' inayoendeshwa na Kampuni ya Bia ya Serengeti kupitia bia yake ya Pilsner Lager, imeanza kwa kishindo huku vijana 'wapambanaji' wakiielezea kama mkombozi wa maisha kwao.

Kampeni hiyo itakayodumu kwa miezi mitatu inalenga kutoa zaidi ya Sh. milioni 50 kwa washindi watano ambao kila mmoja biashara yake itawezeshwa kupitia kupatiwa vitendea kazi vyenye thamani ya zaidi ya Sh.milioni 10.

Kwa mujibu wa Meneja wa chapa wa SBL, Ester Raphael, shindano hilo ni mahusus kwa ajili ya vijana wapambanaji wanaofanya shughuli mbalimbali kama ukulima, uvuvi, vinyozi, waendesha boda boda na wengineo, ambao wanatamani kufikia malengo makubwa, lakini wanapata changamoto katika upambanaji wao kutokana na kukosa uwezeshwaji hali inayowapunguzia kasi ya kufikia malengo yao na mafanikio kwa wakati.

Ester alisema: "Pilsner ni bia ya vijana wapambanaji, wasiokata tamaa na wenye kiu ya kufikia mafanikio makubwa. Tumeona ni vyema kuwawezesha wateja wetu ambao wana kiu ya kufikia mafanikio kwa kuwapa vitendea kazi ili wazidi kusonga mbele zaidi."



Baadhi ya vijana wajasiriamali wadogo wadogo wamesema kampeni hiyo itakuwa msaada mkubwa kwao kutokana na wengi wao kukabiliwa na changamoto ya upatikanaji wa mitaji kwa ajili ya kupanua biashara zao.

Hamisi Mdindile, ambaye ni dereva bajaji anayefanya shughuli zake eneo la Kimara Mwisho jijini Dar es Salaam, amesema anaiona kampeni hiyo kama mkombozi kwa vijana wapambanaji kutokana na mazingira magumu ya kupata mitaji

Kwa upande wake, Frank Mosha, ambaye ni fundi wa kutengeneza mageti katika eneo la Pasua mjini Moshi, anasema ameanza kuweka wazo lake la kibiashara vizuri ili kujihakikishia ushindi na kupata mtaji wa kukuza biashara yake.

Vigezo vitakavyotumika kupata washindi ni pamoja na umri usiozidi miaka 35 na mshiriki atatakiwa kuwa na biashara isiyozidi miaka miwili na pia kuwa na 'simulizi' ya kuvutia zaidi juu ya namna alivyoanza biashara na wapi anataka kuipeleka biashara hiyo.

"Unachotakiwa kufanya ni kufuatilia matangazo yetu katika vipindi mbalimbali vya redio na utashiriki kwa kupiga namba 0800750203 Bure kisha kufuata maelekezo kutoka timu yetu maalumu ya wataalamu wabobezi, baadaye utaweza kueleza biashara yako na namna ambavyo ungetamani bia yetu ya Pilsner ishiriki katika kukuza biashara yako," alifafanua Ester.

Aliongeza kuwa "kushiriki kwa njia ya baa, nunua bia yako ya Pilsner upate namba ya ushiriki. Mawazo bora matano, yataweza kupitishwa baada ya timu kujiridhisha na uhalisia wa shughuli ikiwamo kuwatembelea wapambanaji hao katika maeneo yao ya kazi.




Mratibu wa Mbio za Uhuru Marathon, Innocent Melleck (katikati), akizungumza na waandishi wa habari wakati wa kutangaza mbio hizo kwa mwaka huu, zinazotarajiwa kufanyika Desemba 9, jijini Dar es salaam. Wengine ni Mshauri wa Ufundi wa Uhuru Marathon na Katibu mstaafu wa Shirikisho la Riadha, Suleimani Nyambui (kushoto) na Mtaribu Mwenza wa Uhuru Marathon, Revocatus Rugumila. **MPIGAPICHA WETU**

# *Msimu mbio za Uhuru Marathon 2021 wazinduliwa*

**Na Mwandishi Wetu**

MSIMU mpya wa mbio za Uhuru Marathon umezinduliwa jana jijini Dar es Salaam huku waandaaji wakieleza kuzitumia mbio hizo kukusanya fedha kwa ajili ya kujenga kituo cha riadha.

Mbio hizo ambazo zitafanyika Desemba 9, mwaka huu zitaanzia na kumalizikia kwenye viwanja vya Leaders, Dar es Salaam.

Mratibu wa mbio hizo, Innocent Melleck, alisema msimu huu wanariadha zaidi ya 5,000 kutoka ndani na nje ya nchi watachuana.

Alisema kila msimu wa mbio hizo, watakusanya Sh. bilioni moja kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha michezo ambacho kitajengwa kwa miaka minne hadi kukamilika.

"Sehemu na mkoa gani kituo hicho kijengwe utafanywa na jopo la wataalamu likiongozwa na Suleiman Nyambui, ambaye ni kocha wa kimataifa wa riadha," alisema Melleck.

Amesema tofauti na mbio zingine nchini, msimu huu mbio za Uhuru Marathon zitakuwa na wakimbia wa marathon, nusu marathon, kilomita 10, tano na tatu ambazo zitakuwa za viongozi mbalimbali.

"Pia tutakuwa na mbio za kilomita 2.5 maalumu kwa ajili ya watoto," alisema Melleck.

Nyambui ambaye ndiye Mkurugenzi wa ufundi wa mbio hizo, alisema kitendo cha kuweka mbio za watoto ni mwanzo mzuri wa kuwaandaa vijana wadogo kuwa na msingi bora kwenye riadha.


"Walichonifurahisha ni mpango wa waandaaji kufikiria kujenga kituo, popote duniani huwezi kufanikiwa kwenye michezo bila kuwa na kituo cha michezo," alisema.

Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu, ndiye ameombwa kuwa mgeni rasmi kwenye mbio za msimu huu, mwaka 2014 wakati zinaanza, Rais mstaafu kwa sasa, Jakaya Kikwete ndiye alikuwa mgeni rasmi.

Michezo

Alhamisi Agosti 19, 2021

Nipashe



Ronaldo aja juu madai kuachana na Juventus UKURASA 22

# MUKOKO AZUA HOFU, NABI AFUNGUKA

●●● Asifu kusajiliwa mafundi kila idara, asema kilichobaki sasa ni kuhakikisha wanapambana kufika...

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

WAKATI hofu ikitanda kwa baadhi ya wanachama na mashabiki wa Yanga baada ya kutoonekana picha za kiungo mkabaji wa timu hiyo raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo akiwa mazoezini na wenzake nchini Morocco, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Nasreddine Nabi, naye amefunguka mengi kuhusu kikosi chake.

Yanga ambayo imeweka kambi mjini Marrakesh, Morocco kujiandaa na msimu mpya wa Ligi Kuu Bara na michuano ya kimataifa, ilisafiri na kikosi chake cha wachezaji 29 akiwamo Mukoko ambaye mashabiki wengi wameingiwa na hofu huenda ameuzwa kutokana na kutoonekana katika picha za mazoezi zinazosambaa mitandaoni.

Lakini Ofisa Habari wa klabu hiyo, Hassan Bumbuli, akizungumza na Nipashe jana, amewataka mashabiki hao watulie kwani yupo na anafanya mazoezi na wenzake kama kawaida.

Wanachama na mashabiki wengi wa Yanga wameonekana kushangazwa na kutoonekana kwenye picha yoyote ile ya video na mnato kwa mchezaji huyo mazoezini nchini Morocco ambako timu hiyo imepiga kambi kwa ajili ya kujiandaa na msimu ujao wa Ligi Kuu.

Kwenye mitandao mbalimbali ya kijamii, mashabiki wa timu hiyo wamekuwa na wasiwasi, wakiulizana wenyewe kwa wenyewe ni kwa nini kiungo huyo haonekani.

Mtandao rasmi wa kijamii wa klabu hiyo umekuwa ukichapisha picha za wachezaji mbalimbali na klabu hiyo, lakini kwenye kuchangia, baadhi wanauliza alipo Mukoko kwani hawamwoni.

Akizungumzia suala hilo, Bumbuli alishangazwa na madai hayo na kuwataka Wanayanga kutulia kwa kuwa mchezaji huyo bado ni mali ya Yanga na yupo kambini na wenzake.

“Ukiangalia ile picha utamuona Mukoko, yeye ndiye anayewafundisha wenzake kucheza, labda tu kwa vile hajaonekana kuchapishwa kwenye ‘peji’ (kurasa) ya klabu, lakini yupo na bado ni mali ya Yanga, nawaambia tu mashabiki wasiwe na wasiwasi,” alisema Bumbuli.

Wakati huo huo, Kocha Mkuu wa Yanga, Nabi amefurahishwa na kazi ya usajili uliofanywa na uongozi wa klabu hiyo na kueleza kwamba na jukumu kubwa la kutimiza malengo yanaotarajiwa kwenye Ligi Kuu na michuano ya kimataifa itakayoanza Septemba 10, mwaka huu.

Nabi alimwambia mwandishi wetu kuwa, amefurahi kuona viongozi wamefanyia kazi mapendekezo yake, hivyo atahakikisha wanapambana kutafuta matokeo mazuri kuanzia kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa.

Alisema usajili uliofanywa umefuata vigezo vyote alivyopendekeza katika ripoti yake na ana imani kila kitu kimeenda sawa na sasa wataingia katika mapambano ya kushinda katika mechi yao ya awali dhidi ya Rivers United ya Nigeria.

“Usajili umelenga vigezo ikiwamo kuimarisha safu yetu ya ulinzi kwa kusajili mabeki wa pembeni, ninaimani nao watakuja kuongeza uimara wa kuzuia na kuifanya timu yetu kutofungika kwa urahisi, tunajipanga vizuri kuhakikisha tunafikia malengo yetu,” alisema kocha huyo.

Mkurugenzi wa Kamati ya Mashindano ya Yanga, Thabiti Kandoro, alisema baada ya kikosi kuwasili nchini Morocco kila kitu kimeenda sawa na sasa kocha Nabi anaendelea na majukumu ya kuandaa kikosi.



Beki mpya wa Yanga, Shaban Djuma, akiwa mazoezini kwenye kambi ya timu hiyo nchini Morocco. **PICHA: YANGA**

## Simba yashusha jembe jipya tena

**Na Tunu Hassan, TUDARCo**

MABINGWA watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara na Kombe la FA, Simba wamezidi kujiimarisha kuelekea msimu mpya baada ya jana kutambulisha kiungo mshambuliaji mpya, Jimmyson Steven Mwanuke.

Mwanuke mwenye umri wa miaka 18, ambaye msimu uliomalizika wa Ligi Kuu Bara alikuwa nguzo muhimu katika kikosi cha Gwambina FC iliyoshuka daraja, anakuwa mchezaji wa nne mzawa kutambulishwa msimu huu kutumikia mabingwa hao wa nchi.

Wengine ni Israel Mwenda, Yusuph Muhilu, Abdulsamad Kassim Ali, ambao tayari wapo na timu hiyo kambini nchini Morocco wakijiandaa na msimu mpya.

Mwanuke ambaye anacheza nafasi ya winga, inaelezwa kuwa amepata dili la miaka mitatu la kuwatumikia Simba, hivyo ni mali ya miamba hiyo hadi mwaka 2024.

Mbali na wachezaji hao wazawa, pia Simba imesajili nyota wanne wa kimataifa, viungo; Wamalawi Peter Banda na Duncan Nyoni, beki Henock Baka ‘Varane’ kutoka DR Congo, Pape Ousmane Sakho raia wa Mali.

Simba inayonolewa na Kocha Mkuu, Didier Gomes, imewapoteza viungo wake wawili; Mzambia Clatous Chama aliyesajiliwa na RS Berkane ya Morocco na Luis Miquissone raia wa Msumbiji anayetarajiwa kujiunga na mabingwa wa Afrika, Al Ahly.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >